# Nipashe

Jumatatu Agosti 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581031
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,019,301,493/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Chongolo** awashukia viongozi wanaotaka kumchonganisha...

UKURASA 3




UKURASA 12



# Wakenya kuamua Ruto, Odinga kesho

• **Wenyewe** waahidi kukubali matokeo uchaguzi ukiwa.... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4
RIPOTI MAALUM -2
**SHULE YENYE MAZINGIRA HATARISHI KWA WALIMU, WANAFUNZI NA ELIMU**
KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na ufafanuzi wa namna ya kufika shuleni Kiboriani wilayani...

UKURASA WA 5
**MGOGORO WA NCCR-MAGEUZI NGOMA NZITO**
MWENYEKITI aliyesimamishwa uongozi, James Mbatia, amesema wiki hii ataitisha mkutano na vyombo...

## Saratani ya damu yawatesa watoto, 500 hupokelewa kila mwaka MNH

UKURASA 3




Rais Samia Suluhu Hassan akifungua kitambaa kuashiria uzinduzi wa majengo mapya ya Chuo cha Ualimu Mpuguso wilayani Rungwe mkoani Mbeya jana. **PICHA: IKULU**

# Samia ahimiza ushirikiano wa kibiashara mpakani

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SC HAIJAWAHI KUTOKEA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Raila, Ruto watupa karata za mwisho

**Maulid Mmbaga na Novatus Makunga**

WAKATI ikibaki siku moja kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu nchini Kenya, miongoni mwa wagombea wa urais akiwamo Naibu Rais, William Ruto na Raila Odinga wamesema watakubali matokeo ya uchaguzi endapo upigaji wa kura utakuwa huru na wa haki.

Akizungumza na wananchi juzi katika mkutano wa mwisho wa kampeni katika uwanja wa Nayo, Naibu Rais Ruto, pia aliahidi kukabiliana na ufisadi iwapo muungano wake wa Kenya Kwanza utashinda uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika kesho.

Ruto alisema kwamba wao pekee ndiyo walio na mpango thabiti wa kukabiliana na janga la ufisadi nchini humo.

"Sisi ndiyo timu pekee ambayo inaweza kupambana na kutekwa nyara kwa taifa, washindani wetu hawana mpango maalum kuhusu kukabili ufisadi, isitoshe tatizo na 'handisheki' ni kuwa iliunda mfumo ambao uliwezesha taifa kushikwa mateka na rahisi kwa ufisadi kudumu," alisema Ruto.

Aliongeza kuwa yuko radhi kushiriki kikombe cha chai na mgombea wa urais wa Muungano wa Azimio la Umoja One Kenya, Raila Odinga ambaye ni mpinzani wake mkuu.

Aidha, alibainisha kuwa hakuna uhasama kati yake na Raila, na kwamba yuko tayari kukutana naye uchaguzi utakapokamilika.

"Nimemwambia rafiki yangu Raila ya kwamba mimi niko tayari kunywa na yeye chai baada ya Jumanne. Chai tutakunywa rafiki yangu, kwa sababu sisi ni Wakenya na kwa sababu sisi ni ndugu," alisema Ruto.

**ODINGA: AZIMIO ITAINUA WAKENYA**

Odinga alisema serikali ya Azimio la Umoja One Kenya itajenga viwanda na kuinua maisha ya Wakenya kwa kutengeneza nafasi za ajira.

"Zimebaki saa chache kufikia uchaguzi, tupige kura mapema na tushinde mapema, Azimio la Umoja tunasimama na Wakenya, tembeeni na sisi pamoja, pia amkeni alfajiri na kupiga kura kwa Azimio," alisisitiza Odinga.

**KENYATTA AMPIGIA PANDE ODINGA**

Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, anayemaliza muda wake, wakati akizungumza na wananchi wa Mt Kenya mjini Nyeri, aliwaeleza wakazi hao kuwa huenda wakabaki upinzani iwapo hawatamchagua Raila Odinga.

Alisema kwamba Raila ndiye ataibuka mshindi wa uchaguzi unaotarajiwa kufanyika kesho.

Pia aliwaambia Mt Kenya kuwa Raila ataibuka mshindi hata kama hawatamuunga mkono mwenyekiti huyo wa Azimio, huku akihimiza kuwa wagombea wa Azimio wachaguliwe ili nao wawe serikalini.

"Mniamini au mkose, mchezo huu mshindi atakuwa ni Raila na Martha, chagueni viongozi walio katika muungano wa Azimio," alisema.

"Nimekuja kuwaambia kwaheri na pia nizungumzie uongo ambao mliambiwa kunihusu, mlidanganywa kuwa nataka kusalia mamlakani kupitia BBI, lakini kile nilikuwa nataka ni eneo la Mt Kenya kufurahia mgao zaidi wa mali ikilinganishwa na maeneo ambayo idadi ya watu iko chini," alisema.

**WAANGALIZI 52 WATUA KENYA**

Katika kuhakikisha kuwa uchaguzi huo unaenda vizuri Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC) pia imepeleka waangalizi 52 katika Uchaguzi Mkuu wa Kenya.

Kiongozi wa timu ya waangalizi hao Dk. Jakaya Kikwete, alisema walipata mafunzo ya siku tano ya miongozo ya kimataifa ya uchunguzi wa chaguzi kuu za nchi.

Dk. Kikwete ambaye ni Rais mstaafu wa Tanzania alibainisha kuwa jumla ya waangalizi 52 wa uchaguzi kutoka nchi na wanachama wa EAC wanaogawanyika katika makundi 15 wakiwamo kutoka Bunge la Afrika ya Mashariki (EALA), watakuwa waangalizi wa uchaguzi mkuu huo wa Kenya.

Alisema majukumu ya waangalizi hao ni kufuatilia suala zima la kampeni, upigaji kura, usimamizi wa vituo vya kupigia kura, ujumlishaji wa matokeo na kutangazwa kwake.

**YAONYA UNYANYASAJI WANAWAKE**

Shirikisho la Kimataifa la Haki za Kibinadamu (FIDH) na Tume ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KHRC) zimeonya kuhusu unyanyasaji dhidi ya wanawake kuelekea uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika kesho nchini Kenya.

Mashirika hayo yalibainisha kuwa katika ghasia zilizojitokeza wakati wa uchaguzi wa mwaka 2017, KHRC iliorodhesha kesi 201 za unyanyasaji wa kijinsia, lakini hadi leo hakuna hatua iliyochukuliwa na serikali kuhakikisha waathiriwa wanapata haki zao.



Mkazi wa Ipinda wilayani Kyela mkoani Mbeya, akishangilia hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kufungua barabara ya Likusya-Ipinda-Matema yenye kilometa 39 jana. **PICHA: IKULU**

# Wamshukuru Rais kulipa malimbikizo

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

HALMASHAURI ya Mji wa Babati mkoani Manyara imemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupandisha madaraja ya watumishi 680 na kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi 358 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Taarifa ya serikali ya kupandisha madaraja na kulipa malimbikizo ilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Anna Fissoo, wakati wa mahojiano maalum na Nipashe. Alisema kwa mwaka wa fedha 2021 watumishi 380 walipandishwa madaraja na mwaka 2021/2022 walipandishwa madaraja watumishi 300.

Alisema watumishi 358 walilipwa malimbikizo ya mishahara yao na zaidi ya Sh. milioni 371 zililipwa na serikali.

Mkurugenzi huyo alifafanunua kuwa katika nyongeza ya mshahara, watumishi 1,411 wameongezewa mishahara katika halmashauri hiyo. "Mtumishi akipandishwa daraja kuna kiasi cha fedha kinaongezeka kwenye mshahara wake na anakuwa na morali ya kufanya kazi," alisema Fissoo.

Naye Mwalimu Theofilida Martine, akizungumza na Nipashe alisema wana mategemeo makubwa na Rais Samia na wanamshukuru kwa nyongeza ya mshahara.

Naye Katibu wa Wafanyabiashara Wakulima na wenye Viwanda (TCCIA) mkoa wa Manyara, Mwanahamisi Hussein, akizungumzia serikali alisema miundombinu ya barabara imeendelea kuboreshwa na kuwafanya waweze kufanya biashara vizuri.

# Samia ahimiza ushirikiano kibiashara mpakani

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameagiza Kituo cha Pamoja cha Forodha kati ya Tanzania na Malawi kilichoko Kasumulu wilayani Kyela, mkoani Mbeya kuendelea kutumika wakati maboresho yakiendelea ili biashara pande zote zisikwame.

Amesisitiza mizigo yote inayopitishwa mpakani humo kwa kufuata taratibu za kisheria isizuiliwe ili kukuza biashara na uchumi.

Alikuwa akizungumza jana na wananchi wa Kasumula wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hicho na kusema ni lazima kila mzigo unaostahili kulipiwa ushuru ukalipiwa kabla ya kuvushwa ili kutoikosesha nchi mapato, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi mikoa ya Mbeya na Songwe.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha huduma za wananchi zinaboreshwa na kuimarisha ushirikiano baina ya nchi hizo hasa wa kibiashara kutokana na ujirani wa muda mrefu.

Aliwataka wasimamizi wa kituo hicho kuhakikisha wanafanyakazi kwa kuzingatia sheria ikiwa ni pamoja na kuhakikisha usalama wa watumiaji wa kituo hicho unakuwa imara.

"Nawapongeza sana wote walioshiriki kwenye ujenzi wa kituo hiki wakiwamo mkandarasi, mhandisi mshauri pamoja na viongozi wa serikali ya mkoa wa Mbeya kwa usimamizi mzuri wa kituo hiki, nawaagizeni kituo hiki kiendelee kutumika wakati ujenzi ukiendelea," alisema Rais Samia.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila, alisema mradi huo unajumuisha majengo mbalimbali yakiwamo ya abiria, ofisi za mifugo, ofisi za ukaguzi wa magari, ofisi za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na shughuli zingine muhimu.

Vilevile, alisema mradi huo unajumuisha eneo la maegesho ya magari ambayo yanasubiri ukaguzi pamoja na barabara mbalimbali za kuingia na kutoka kwenye eneo hilo.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 24, umeajiri zaidi ya Watanzania 300 kwenye kazi mbalimbali na kwamba ujenzi umefikia asilimia 87.

"Mradi huu ni sehemu ya uboreshaji wa mazingira ya kibiashara kwenye ushoroba wa Afrika kutoka Kaskazini kwenda Kusini kwa ukanda huu miradi ya aina hii ni miwili ukiwamo pia wa Tunduma," alisema Mativila.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema kituo hicho ni muhimu kwa maendeleo ya mataifa yote mawili kutokana na mwingiliano mkubwa wa kibiashara baina ya mataifa hayo.

Aidha, aliomba linunuliwe gari la zimamoto kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya moto kusaidia wananchi wa Wilaya ya Kyela.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, alisema serikali ina mpango wa kununua magari ya zimamoto kwa ajili ya maeneo mengi, ikiwamo kituo hicho ambalo litanunuliwa kabla ya kukamilika kwake na halmashauri.

Katika ziara yake Rais Samia alitembelea halmashauri mbili za Rungwe na Kyela na kuweka mawe ya msingi katika miradi na kuzungumza na wananchi.

Aliweka mawe ya msingi kwenye miradi ya ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Forodha cha Kasumulu na ukarabati wa Chuo cha Walimu cha Mpuguso na kuzindua barabara ya Kikusya-Ipinda-Matema ambayo imekamilika na inaendelea kutoa huduma.

Aidha, Rais anatarajiwa kuhutubia wakulima na wadau mbalimbali kwenye maadhimisho ya Siku ya Wakulima Nanenane leo katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya.




Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Daniel Chongolo, akizungumza na viongozi wa CCM Wilaya ya Same baada ya kupewa heshima ya kuwa Mzee wa Kipare wakati wa ziara ya kukagua, kuhamasisha na kuhimiza utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2020-2025 kwenye ukumbi wa Joyland, Same mkoani Kilimanjaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chongolo: Sitawavumilia viongozi wanaoshindwa kutekeleza miradi

**Na Mary Geofrey,** SAME

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amesema watendaji wanaoshindwa kutekeleza miradi ya maendeleo wanamchonganisha na Rais Samia Suluhu Hassan na wananchi na kwamba hatawavumilia.

Alisema CCM hakipo tayari kuendelea kujibu hoja za wananchi katika miradi ambayo Rais Samia ameahidi kuifanya na watendaji wake wapo kimya.

Sekta ambayo Chongolo alikuta miradi yake ina changamoto katika Mkoa wa Kilimanjaro ni maji, barabara, afya na umeme.

Chongolo aliyasema hayo akiwa wilayani Same mkoani Kilimanjaro, wakati akihitimisha ziara ya siku tano mkoani humo kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhimiza sensa ya watu na makazi.

Alisema akifika jijini Dodoma atawaita wabunge wawatajie miradi ambayo haijatekelezwa licha ya Rais Samia kuagiza ifanyike na kuwakutanisha na mawaziri husika, ili waeleze nini mipango yao katika hilo.

"Tunataka mpango wa kina unaoeleza ni lini mradi huo utakamilika, hatutaki maneno maneno, mwaka wa kwanza, wapili, wa tatu wa nne...halafu ninyi wasaidizi mpo ofisini hamumsaidii kazi, maana yake hampo tayari kumsaidia na kumchonganisha na wananchi," alisisitiza Chongolo.

Kwa mujibu wa Chongolo, yeye ni msaidizi wa Rais wa upande wa pili (chama), hayupo tayari kuvumilia tatizo hilo.

Alisema katika wilaya nyingine za mkoa huo alikutana na changamoto ambazo zinahitaji msukumo wake na ataifanya kazi kabla ya kuja kuhojiwa na wananchi mwaka 2025.

**AWESO ATAKIWA KUKAMILISHA MRADI**

"Niwahakikishie wiki mbili zijazo nikiwa Dodoma nitaanza na Waziri wa Maji, aje atuambie na tutaita Mbunge wa Mwanga, Korogwe na Same Mashariki, tukae wote atuambie ana mpango gani wa kumaliza huu mradi na uzuri wake akija na mpango unaobabaisha mimi ni bosi wake, mnavyoniona mnafikiri mimi ni wa mchezo mchezo eh! Subirini sasa muone mbunge wenu atawarudishia majibu," alisema huku akishangiliwa na wananchi.

Alimtaka Waziri Aweso kupeleka wataalam wa kuchimba visima viwili vya maji, Wilaya ya Same ili kupunguza makali ya wananchi kukosa maji kwa zaidi ya miaka 10 wakati wakisubiri kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe.

Mradi huo unaotarajia kukamilika baada ya miezi sita ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Nne ambao unagharimu Sh. bilioni 262 na ukikamilika utahudumia wananchi 400,000.

Alimtaka Aweso kutekeleza ahadi yake ya kuwachimbia kisima kimoja wananchi hao, ambayo hajaitekeleza hadi anafika wilayani hapo.

"Sasa badala ya kuja kuchimba kisima kimoja njoo uchimbe visima viwili nami nakupa siku nne uhakikishe hayo magari ya kuchimba yamefika hapa Same," alimuagiza Aweso.

Aliitaka kamati ya maendeleo wilaya ya Same kusimamia utekelezaji wa mradi huo wa visima ili wananchi wapate huduma wakati wakisubiri mradi maji ambao utakamilika miezi sita ijayo.

Naye, Aweso aliahidi kutekeleza agizo hilo la Chongolo kwa wakati ili kuhakikisha wananchi wa Same wananufaika na huduma hiyo.

Aliahidi kupewa siku moja kwa ajili ya kuanza huduma hiyo ya kuchimba kisima ili wananchi waanze kunufaika na huduma za maji wakati wakisubiri kukamilika kwa mradi huo.

Kuhusu mradi huo mkubwa wa maji, alisema wataalam wapo kazini wanaendelea kufanya kazi na wanatarajia utakamilika miezi sita ijayo na kuukabidhi kwa wananchi.

Januari 19, mwaka jana, serikali ilikabidhi mradi huo wa maji kwa Mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) baada ya kusitisha mkataba na wakandarasi waliokuwa wakitekeleza mradi huo ulioasisiwa na Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete.

Mradi huo ulikuwa ukitekelezwa na wakandarasi wawili ambao ni M.A Kharafi & Sons na kampuni ya Badr East Africa Enterprises na wote walisitishiwa mkataba mwishoni mwa mwaka 2020 kutokana kusuasua.

Baada ya DAWASA, kukabidhiwa mradi huo, iliahidi hadi kufikia Novemba 30, mwaka jana ungekuwa umekamilika na ungezinduliwa.

Mradi huo una uwezo wa kuzalisha zaidi ya lita milioni 65 kwa siku.

Mwaka 2010 Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, aliahidi kujengwa kwa mradi huo wa kutoa maji Bwawa la Nyumba ya Mungu wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu 2010, lengo likiwa ni kutatua kero ya muda mrefu ya maji katika wilaya za Mwanga na Same mkoa Kilimanjaro na baadhi ya vijiji vya Wilaya ya Korogwe Mkoa wa Tanga.

# Watoto 500 saratani ya damu hupokelewa kila mwaka MNH

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI wa watoto aliyebobea katika magonjwa ya saratani na damu, Lulu Chirande, amesema kila mwaka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) inapokea wastani watoto wapya 500 wenye saratani.

Aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Global Hope wenye lengo la kusaidia kuwezesha matibabu ya watoto wenye saratani na matatizo ya damu unaofanyika katika ngazi tatu.

Dk. Chirande alisema watoto wengi hufikishwa hospitalini hapo wakiwa wamechelewa na zaidi ya asilimia 60 ya wanaowatibu, huwa katika hatua ya tatu na ya nne ambayo uwezekano wa kupona ni mdogo.

"Tatizo hili la saratani ni kubwa zaidi ikilinganishwa na idadi hii ya watoto wanaofika hospitali na kufanyiwa utafiti na kuambiwa wana saratani, asilimia kubwa hawafanikiwi kufika katika hospitali zenye utaalamu wa kutosha," alisema.

Mtaalamu huyo alisema tatizo la saratani kwa watoto liko zaidi katika nchi za Afrika, Kusini mwa Afrika na nchi za Asia.

"Maeneo hayo ndiyo watoto walipo, sio kwamba sehemu hizo watoto wanapata saratani zaidi, ndiko watoto walipo wengi wenye umri chini ya miaka 18.

"Asilimia 80 hadi 90 ya watoto wanaopata saratani ulimwenguni, wanatokea katika hizi nchi za uchumi wa chini na uchumi wa kati na kwa wastani, inakadiriwa kama watoto 300,000 kila mwaka ulimwenguni wanapata saratani," alisema.

Dk. Chirande alisema, kwa upande wa Tanzania kila mwaka watoto 800 hupata saratani na hiyo ni idadi ya wale wanaofikishwa hospitali kuchunguzwa na kugundulika.

"Uwezo wa kutoaji huduma una changamoto, hivyo vita vinakuwa vigumu, changamoto nyingine ni dalili za saratani ni nyingi ukiondoa zile saratani zenye uvimbe zinazofanana na magonjwa mengi. Mzazi akiona mtoto wake anaumwa amwahishe kituo cha afya."

"Kwa upande wetu, watoa huduma katika vituo vya afya wanatakiwa wawe na uelewa wa kugundua," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Tiba, Dk. Omary Ubuguyu, alisema programu hiyo ni kwa ajili ya wataalamu wanaojengewa uwezo wa kutambua na kutibu.

Pia ina lengo la kuongeza upatikanaji wa dawa kwa watoto wenye saratani na magonjwa mengine ya damu.

Makamu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Prof. Andrea Pembe, alisema wameshirikiana na Global Hope kuanzisha programu hiyo ambayo itafundisha madaktari kwa ngazi ya Uzamivu na Udhamili katika matibabu ya satarani ya damu kwa watoto.

Naye Mkurugenzi wa Global Hope Program kutoka Texas Children Hospital USA, Dk. David Poplack, alisema wataendelea kushirikiana katika eneo la mafunzo, utafiti, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa ajili ya maisha ya watoto wenye saratani.

## KIBORIANI

# Shule yenye mazingira hatarishi kwa wanafunzi, walimu na elimu

Na Sanula Athanas

**KATIKA sehemu ya kwanza ya ripoti hii jana, kulikuwa na ufafanuzi wa namna ya kufika shuleni Kiboriani wilayani Mpwapwa na ushuhuda wa hali mbaya ya miundombinu ya madarasa na vyoo vya shule hiyo. Endelea na sehemu ya pili kupata undani wa kinachojiri huko.**



Mwalimu wa Mazingira, Afya na Michezo katika Shule ya Msingi Kiboriani wilayani Mpwapwa, akionesha moja ya nyumba zinazotumika kwa makazi ya walimu shuleni hapo. **PICHA: SANULA ATHANAS**

**MAISHA YA WALIMU**

Ili taaluma ifanyike shuleni, kuwapo kwa walimu ni sehemu ya maisha. Aya ya 3.4.1 ya Sera ya Taifa ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inahimiza kuwapo usimamizi wa rasilimali watu kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya elimu.

Moja ya malengo ya sera hiyo ni kuhakikisha ifikapo mwishoni mwa mwaka huu (2022), lengo la uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi la 1:45 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45) linatimia. Hali ikoje Kiboriani?

Mwalimu Mkuu Kasanda anaanza kwa kulalamika juu ya anachokiita mwenyewe 'kitendawili' akiwa na walimu wanne hivi sasa kazini, wanaopaswa kufundisha madarasa manane (likiwamo la awali).

Anasema mwalimu mwingine mmoja ni mgonjwa na hajarejea kazini kwa takriban mwaka mmoja sasa baada ya kupata ajali ya pikipiki iliyokuwa ikipanda mlima katika safari ya kutoka mjini Mpwapwa kuelekea kazini kwake Kiboriani.

Mwalimu Kasanda ambaye hafichi masononeko yake, anaendelea: "Kuna shida ya uhaba wa walimu ambayo mimi kiutendaji inanipa mazingira magumu. Kwa sasa tupo walimu watano tu hapa shuleni, mimi (mwalimu mkuu) nina majukumu mengi ya kiutawala, hivyo unaona hali yetu kiutendaji ilivyo.

"Hapa hatuna mwalimu wa kike, ni tatizo kubwa kwetu linapokuja suala la kuwasaidia watoto wa kike walioanza kupevuka. Kuna baadhi ya matatizo yao tunayatatua na mengine tunayashindwa. Kuna dada hapa kijijini anatusaidia, tunamtumia kutoa elimu rika kwa watoto wa kike.

"Tumeshatoa taarifa na tunazidi kutoa taarifa kwa ngazi za juu serikalini kuwaarifu kwamba 'jamani huku kuna shida'. Athari za kiafya ni kubwa, tukianzia kwenye hali ya hewa kwa walimu wangu, wengi ni wageni, siyo wenyeji wa huku."

Hata hivyo, Ijumaa iliyopita Nipashe ilipozuru kwenye Shule ya Msingi Kikombo iliyoko kilomita mbili kaskazini mwa Mji wa Mpwapwa, ilibaini kuwapo idadi kubwa ya walimu shuleni hapo kulinganishwa na majirani zao Kiboriani.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kikombo, Anusiata Cornel (49), shule yake kwa sasa ina walimu 13 (wa kike 10) wanaofundisha wanafunzi 306, sawa na uwiano wa 1:24 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi 24), takwimu zinazotoa ishara ya kutokuwapo msawazo katika upangaji wa walimu wa shule za msingi wilayani Mpwapwa.

Mwalimu Mkuu Kasanda anaendelea na ufafanuzi kuhusu madhila yanayowakumba walimu wa Shule ya Msingi Kiboriani, akisema: "Hali ya hewa ya huku ni ngumu sana. Bahati nzuri leo mmefika hapa mmekuta jua limewaka kidogo, lakini ninaamini mmeelewa kwamba hali ya huku ni balaa kwa baridi. Hali ya kiafya ni shida kwa walimu wangu.

"Tuna nyumba moja tu hapa kwa ajili ya walimu. Hizo nyingine ni vibanda tu ambavyo wanakijiji wametengeneza kwa ajili ya kujishikiza.

Sasa kwa mtumishi wa serikali, mwalimu ambaye anatakiwa aamke asubuhi yuko vizuri, aingie darasani amsaidie mtoto, anatoka kwenye nyumba ambayo anasononeka moyoni.

"Kiuhalisia siyo nzuri kabisa. Viko vibanda vinne ambavyo tunakaa kwa kujibanza hivyo hivyo, lakini mtu unakuwa na masononeko moyoni."

Mwalimu Mkuu Kasanda anasimulia zaidi kwamba walimu wamebuni staili ya kuishi, akisisitiza "maisha lazima yaendelee", wote wameziwekea familia zao makazi mjini Mpwapwa, nao wakibuni mfumo wa maisha kila Ijumaa wanateremka kwa safari ya pikipiki kwenda kwa familia zao mjini na wanarejea Jumapili jioni au Jumatatu mapema kuendelea na kazi.

Anasema mbali na vikwazo hivyo vya kikazi, kijijini hapo hakuna zahanati na huduma nyinginezo za kijamii, zikiwamo za kifedha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, Isaya Chitema (48), ambaye ni mwanakijiji na mhitimu wa shule hiyo mwaka 1988, ana ufafanuzi namna mgonjwa anavyopewa huduma:

"Ukiugua hapa, tuna machela maalum za miti tunakubeba kwenda mjini. Mnapoamua kushuka kwa miguu kwenda mjini, inabidi muwe wengi maana porini kuna fisi, nyani na nyoka wengi."

Kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kiboriani, Ramadhan Mfundo, hadi sasa kuna hatua zimeanza kuchukuliwa za ujenzi wa zahanati ya kijiji, ambayo katika hatua za awali, ujenzi wa boma umekamilika.

Nipashe inapohoji kwa Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, Dismas Pesambili, anakiri kutambua tatizo hilo, akiwa na ufafanuzi kwamba imetengwa bajeti ya Sh. milioni 50 kwa mwaka wa fedha ulioko kuendeleza ujenzi huo wa zahanati.

Pia anaongeza kuwa wametafuta nguvu zaidi toka Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuwasaidia nguvu ya kifedha kukamilisha zahanati hiyo, vivyo hivyo kunusuru hali mbaya ya shule.

**WENYEJI WA SHULE**

Kuna dhana kwamba anayechomwa na mwiba ndiye mwenye maumivu halisi. Leah Sajiro ambaye ni Dada Mkuu na mwanafunzi wa darasa la saba, anaanzisha maelezo yake kwa kurejesha hali ya chooni, ambayo hafichi shaka yake kuhusu kinachomsibu kwamba:

> **"Ukiugua hapa, tuna machela maalum za miti tunakubeba kwenda mjini."**

"Unapoingia chooni unakuwa na wasiwasi maana ni kichafu, kibovu na kinaweza kupomoroka muda wowote, lakini hauna namna kwa sababu kilichoko ni hicho hicho..."

Vilevile, mwanafunzi huyo analalamika madarasa yao kuanzia kwa wadogo zao wa darasa la awali hadi la pili, hawana madawati kabisa, huku darasa la tatu hadi la saba vyumba vyao vina madawati machache, hata wanalazimika kukaa watano hadi sita kwa dawati.

Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu Kasanda, shule hiyo kwa sasa ina jumla ya madawati 55. Sera ya Elimu na Mafunzo inayotumika sasa inahitaji dawati moja litumiwe kwa uwiano wa wanafunzi watatu, hivyo kuifanya Shule ya Msingi Kiboriani kuwa na uhitaji wa jumla ya madawati 140 na hali iliyoko sasa ni upungufu wa madawati 85.

Leah pia analalamika kwamba baadhi ya siku walimu huwa hawaingii darasani kabisa, jambo ambalo Nipashe inapotaka ufafanuzi wa Mwalimu Mkuu Kasanda, anaeleza kwamba ni kutokana na kuelemewa kwa idadi ndogo ya walimu wanaoshindwa kukidhi mahitaji ya madarasa yote manane.

"Hata ningekuwa na walimu wengi, wangefundisha vipi wakati vyumba vya madarasa viko vinne tu? Tunajitahidi sana kukabiliana na tatizo la wanafunzi kukosa vipindi vya masomo," Mwalimu Kasanda anafafanua.

Mwalimu Mkuu huyo pia anafafanua namna anavyowezesha kukidhi mahitaji ya wanafunzi wa madarasa manane ndani ya vyumba vinne, akisimulia ubunifu na mtindo wake:

"Tuna mwalimu mmoja anayefundisha darasa la awali hadi la pili. Wanafunzi wa darasa la awali wanaingia asubuhi, ikishafika saa nne, wa darasa la kwanza na la pili wanaingia na wanafundishwa kwa pamoja. Hao wakubwa wa madarasa ya juu (kuanzia la tatu hadi la saba) ni kama nilivyotangulia kueleza hapo awali."

Mwanafunzi Leah anayerejea orodha ya matatizo yote yaliyotajwa, anadokeza moja ya athari za moja kwa moja zinazowafika wanafunzi ni kuugua baadhi ya maradhi kama tumbo na kifua, pia kutofurahia mazingira ya masomo.

Anahitimisha ufafanuzi wake, akipaza ujumbe wake kwa kauli: "Serikali itusaidie kutatua shida hizi kwa kujenga madarasa, vyoo na nyumba za walimu..."

Ni hoja inayoungwa mkono na Kaka Mkuu shuleni, Alpha Nalinje, anayesoma darasa la saba. Mbali na kuongeza hoja ya uhaba wa vifaa vya michezo, msisitizo wake unazama zaidi katika nyayo za hoja tangulizi za dada yake na walimu wake.

Mzazi Elda Ngewe (45), mama wa wanafunzi wawili walio katika darasa la kwanza na la tatu, sehemu ya kwanza ya malalamiko yake inaangukia katika kilio cha wote kuhusu hali ya choo na mazingira ya shule yasiyo rafiki kiafya.

Hapo anafafanua kwamba wao wanakijiji wamelazimika kuchukua hatua za ziada za kuchimba shimo la choo, lakini wamekwama hatua za kumalizia.

Kama ilivyo kwa mtoto wao Leah, Elda naye anapaza sauti ya kuomba msaada wa kiserikali na wadau kipatikane choo kipya kufuta kilio hicho.

Rodgers Malau (50), mzazi wa kiume mwenye watoto wawili darasa la saba (wa kike na wa kiume), pia binti wa darasa la tano, analia na shida ya uhaba wa walimu, nyumba zao, uhaba wa madawati darasani, bila kusahau kilio kikuu cha wote - hali mbaya ya choo.

"Huduma ya choo ni kama haipo, haya matundu manne yameshabomoka na muda wowote yanasababisha hatari kwa watoto wetu," Malau analalamika.

***ITAENDELEA KESHO**

HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akizungumza na walengwa wa TASAF na wananchi wa Kata ya Mazimbu, Manispaa ya Morogoro baada ya kukagua mradi wa funza chuma unaotekelezwa na Kikundi cha Faraja cha Kata ya Mazimbu ambao ni wanufaika wa TASAF, katika ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa shughuli za TASAF. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgogoro wa uongozi ndani ya NCCR-Mageuzi ngoma nzito

**Na Sabato Kasika**

MWENYEKITI aliyesimamishwa uongozi, James Mbatia, amesema wiki hii ataitisha mkutano na vyombo vya habari kueleza kwa kirefu kuhusu mgogoro unaoendelea ndani ya NCCR-Mageuzi nchini.

Akizungumza na Nipashe iliyotaka kujua hatua inayofuata baada ya kupinga uamuzi wa Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi, alisema katika kikao hicho ataeleza mambo yote ili Watanzania wapate picha halisi.

"Kwa sasa siwezi kuzungumza lolote zaidi ya kukwambia tu kwamba, nitaitisha kikao na kuzungumza na waandishi wa habari ili kuelezea kwa kina kile kinachoendelea ndani ya NCCR-Mageuzi," alisema Mbatia.

Aidha, mwandishi wa habari hizi alimtafuta, Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, ambaye alisema alishindwa kuingilia kati mgogoro huo baada ya Mbatia kuandika barua kwenda kwa waziri ni wanachosubiri ni jibu la kiongozi huyo.

Alisema Mbatia aliandika barua kwa Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu- Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, akimuomba asaidie kutatua mgogoro ndani ya chama hicho.

"Ninasikitika kusema waandishi wa habari walinizushia kuwa nimejitoa katika kusuluhisha mgogoro huo, ukweli ni kwamba hatuwezi kuendelea na usuluhishi wakati mgogoro umefikishwa kwa waziri," Jaji Mutungi alisema.

Alisema ofisi yake itaendelea na usuluhishi baada ya kupata taarifa ya ambacho Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge na Uratibu aliamua kwa kuwashauri wadau wa siasa kuvute subira.

"Ofisi yangu (Msajili) kwa sasa haina cha kufanya kuhusu mgogoro huu zaidi ya kusubiri maelekezo ya waziri na pia inaheshimu katiba ya chama hicho, lakini tunasikitika kuzushiwa kuwa tumejitoa," alisema Jaji Mutungi.

"Julai 21, mwaka huu ilikuwa tufanye kikao cha upatanishi, lakini tukaahirisha baada ya Mbatia kuandika barua kwenda kwa waziri, nasi tunaheshimu uamuzi huo, hadi hapo majibu yatakapopatikana," alisema.

Kadhalika, alisema ni muhimu ofisi yake kujipa muda hadi hapo waziri atakapowajibu, na kwamba majibu hayo ndiyo yatatoa mwanga kuhusu namna ya kusuluhisha mgogoro wa uongozi uliokikumba chama hicho.

Mei 21 mwaka huu, Halmashauri Kuu ya NCCR-Mageuzi ilimsimamisha Mbatia na Makamu Mwenyekiti Bara, Angelina Mtahiwa, kutojihusisha na shughuli zozote za chama hicho.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Martha Chiomba alikaririwa na vyombo vya habari akitoa tamko na kuweka msisitizo kwamba Mbatia hapaswi kujihusisha na jambo lolote linalohusiana na NCCR-Mageuzi hadi atakapoenda kujitetea kwenye mkutano mkuu kutokana na tuhuma zinazomkabili.

# JKCI yatakiwa kujipanua Mloganzila

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameitaka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), kuanza mchakato wa kupanua shughuli zake eneo la Mloganzila, Mkoa wa Pwani kutokana na ukubwa wa eneo lililoko.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizindua Bodi ya Wadhamini ya Taasisi hiyo hafla iliyofanyika kwenye ofisi zake, Hospitali ya Taifa Muhimbili jijini Dar es Salaam.

Ummy alisema itakuwa jambo jema kwa taasisi hiyo kuhamia Mloganzila kwa kuwa kuna eneo kubwa la kutosha hata kwa wagonjwa kufanya mazoezi tofauti na walipo kwa sasa ambalo alisema limebanwa.

"Twendeni Mloganzila mkajenge a brand new cardiac hospital (hospitali mpya ya moyo), hii Mwenyekiti nakupa ifanyie kazi twendeni Mloganzila, wizara tupo tuleteeni dokezo twendeni Mloganzila," alisema Ummy wakati akimwagiza Mwenyekiti wa Bodi ya JKCI, Prof. William Mahalu.

"Hapa tunaweza kuwaachia Muhimbili wakafanya kuwa Private au ya watoto sijui, lakini hapa eneo dogo kwa mfano mmemfanyia mtu upasuaji wa moyo anafanyia wapi mazoezi hapa," alihoji.

Mkurugenzi wa JKCI, Prof. Mohamed Janabi, alisema ni kweli JKCI ina mpango wa kujipanua eneo la Mloganzila ambako tayari wana eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 50,000.

Alisema jengo watakalojenga Mloganzila litakuwa na uwezo wa kulaza wagonjwa 200 kwa wakati mmoja na baada ya kukamilika wataamua lipi liwe la watu wazima na watoto.

Alisema ujenzi wa jengo hilo utafanywa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na China na kila upande utatoa fedha nusu na ilikuwa waanze kujenga siku nyingi, lakini kutokana na janga la COVID lilikwamisha mchakato.

"COVID ilisababisha Wachina wakajifungia na hivyo mradi huu ukakwama, lakini michoro yote iko tayari na jengo litajengwa fedha ikishatolewa na likikamilika tutaamua kati ya JKCI Mloganzila na JKCI Muhimbili lipi liwe maalum kuhudumia watoto na lipi lihudumie watu wazima," alisema Janabi.

Mjumbe wa Kamati ya Utalii wa Tiba, Joseph Kahama, alisema serikali inatumia fedha nyingi kupeleka wagonjwa nje ya nchi wakati Tanzania kuna vifaa vya kisasa na madaktari wabobezi wa matibabu ya aina mbalimbali.

"Nchi nyingi zilizotuzunguka hawana vifaa vya kisasa kama sisi, hivyo tunaweza kuvitumia kutibu watu wetu na wageni kutoka nje na tukaokoa shilingi bilioni tatu zinazotumika kila mwaka kupeleka wagonjwa nje ya nchi," alisema.

# 'Treni ya umeme (SGR) kuwa na uwezo kufua umeme wake'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Reli nchini (TRC), Masanja Kadogosa, ametaja sifa za treni ya kisasa ya mwendokasi (SGR) ni kuwa na uwezo wa kufua umeme wake.

Pia, amesema umeme ukikatika treni hiyo ina uwezo wa kuendelea na safari bila ya nishati hiyo kwa dakika 48.

Kadogosa alitoa ufafanuzi huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu shughuli za TRC na bajeti ya mwaka 2022/23. "Hatuhitaji umeme mwingi katika kuendesha treni hii kwa kuwa treni zetu wenyewe zinafua umeme, kwa hiyo unapowasha treni yenyewe inafua umeme wake." "Treni ya SGR uendeshaji wake ni nafuu utaokoa gharama zaidi ya mara tatu zinazotumika kununulia dizeli kuendeshea treni ya kawaida, hata usalama ni wa hali ya juu kwasababu kuna mfumo ambao unaoweza kusimamisha treni inayosafiri ama kuwasiliana na dereva nje ya treni," alisema.

Aidha, alisema shirika hilo linajenga mfumo wa umeme wa msongo wa kilovoti 220 unaojitegemea kwa ajili ya uendeshaji wa treni hiyo ili kuwa na nishati ya uhakika.

Alisema kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro mfumo huo una urefu wa kilomita 160 umekamilika huku kipande cha Morogoro hadi Makutupora ujenzi wake unaendelea. Kuhusu treni kuanza kazi, Mkurugenzi huyo alisema kwa sasa wapo majaribio ya awali na baada ya hapo mwezi Septemba, mwaka huu TRC na Mamlaka ya Udhibiti watafanya majaribio ya uendeshaji ambayo yatachukua miezi mitatu hadi minne.

"Baada ya mdhibiti ambaye LATRA kujiridhisha kuhusiana na usalama wa usafiri huu na ndio watatoa kibali cha kuanza kusafirisha abiria na mizigo, hii operation trial ikikamilika inawezekana huko Januari au Februari mwakani treni itakuwa imeanza kufanya kazi," alisema. Mkurugenzi huyo alisema baadhi ya mabehewa ni ya ghorofa na madereva wameanza kufundishwa na baadaye watapelekwa nje ya nchi.

Kadogosa alisema katika kukomesha wizi wa mizigo katika treni, SGR zitafungwa kamera za ulinzi za CCTV ili kuona vitu vyote vinavyoendelea ndani na kwenye stesheni zake.

"Mtandao wa SGR utafungua milango ya biashara ndani ya nchi jirani za Rwanda, Burundi, DRC Kongo, Uganda na Kenya," alisema.

Akizungumzia fidia kwa waliopisha ujenzi wa SGR, Kadogosa alisema, hadi Mei mwaka huu, kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro wamelipa zaidi ya Sh. bilioni 120 huku asilimia 65 ikitumika kwa kulipa fidia waliopisha kwa Jiji la Dar es Salaam.

Kadhalika, alisema mwezi Oktoba, mwaka huu wanatarajia kuongeza mabehewa kwa treni ya Delax inayofanya safari zake Kigoma kutokana na kubaini uwapo wa uhaba wa mabehewa.

"Kwa Dodoma tutafanya kitu kizuri ambacho kitabadili kabisa taswira ya Jiji la Dodoma, wakati ukifika tutawajulisha ni kitu gani mtakiona," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matamasha Simba, Yanga yaanzie mikoani kilele Dar

**WAKATI** Klabu ya Yanga iliadhimisha kilele cha Wiki ya Mwananchi Jumamosi iliyopita, watani wao wa jadi, Simba leo wataadhimisha Tamasha lao maarufu kama Simba Day lililoasisiwa miaka 13 iliyopita chini ya aliyekuwa Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Dalali.

Jumamosi Yanga iliadhimisha tamasha lao hilo maarufu kama Siku ya Mwananchi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, likiwa ni la nne tangu liasisiwe katika klabu hiyo ya mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam. Kwa ujumla tamasha hilo lilifana na si hilo tu bali kila mwaka klabu hizo zimekuwa zikiboresha matamasha yao hayo kwa kuja na vionjo tofauti ambavyo huwa vivutio vikubwa kwa mashabiki wa soka ndani na nje ya nchi, jambo ambalo kusababisha Uwanja wa Mkapa kufurika.

Pamoja na mambo mengi mazuri na ya kuvutia ambayo hufanyika wiki moja kabla ya kilele cha matamasha hayo, kubwa ambalo Nipashe tumekuwa tukivutiwa nalo ni namna ambavyo klabu hizo hufanya shughuli za kijamii ikiwamo kurudisha kidogo walichokipata msimu mzima kwa kusaidia wasiojiweza na wenye mahitaji maalum.

Hilo hufanyika likiambatana na viongozi, wanachama na mashabiki wa klabu hizo kujitokeza kujitolea damu kwa ajili ya kwenda kusaidia wagonjwa wenye hitaji hilo katika hospitali mbalimbali, kwani zoezi hilo hufanywa na wapenzi wa klabu hizo kote nchini.

Kinachotufurahisha zaidi ni mwitikio mkubwa kwa wanachama na mashabiki wa timu hizo kote nchini, kwani wiki ya matamasha hayo inapotangazwa matawi ya klabu hizo katika mikoa na wilaya mbalimbali hujikusanya na kuanza kufanya shughuli hizo za kijamii kwa kutoa misaada na kuchangia damu, jambo ambalo tunaona ni zaidi ya upendo, hivyo hatuna budi kuwapongeza.

Hata hivyo, tunatamani kuona wigo mpana zaidi kwa klabu hizo kwa sasa kufikiria matamasha hayo kuanzia mikoani na kisha kielele chake kufanyika Dar es Salaam ili kuzifikia jamii kila kona nchini lakini pia wanachama na mashabiki wa timu hizo kufurahia burudani zaidi mubashara.

Tunatambua haitakuwa rahisi kwa klabu hizo kupeleka matamasha hayo kila mkoa hasa kutokana na maandalizi ya msimu mpya kuwa mdogo, hivyo kwa kuanza zinaweza kufanya kwa kanda moja moja mfano mwaka ujao Kanda ya Ziwa, unaofuata Kanda ya Kati, kisha Kanda ya Kaskazini na nyinginezo.

Tunaamini inawezekana kabisa kwa klabu hizo kila moja kufanya matamasha makubwa mawili moja katika kanda moja kabla ya kilele kufanyika Dar es Salaam, jambo ambalo si tu litaziingizia mapato makubwa bali litasaidia pia kuzifikia jamii ambazo zinahitaji nazo kusaidiwa kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa Dar es Salaam.


Ni wazi matamasha hayo yakifanyika klabu hizo zinaweza kuandaa utaratibu mzuri wa kuuza jezi na bidhaa nyingine za klabu kwa wingi, mbali na mapato ambazo zitaingiza kwa mashabiki wao kuhudhuria uwanjani siku hiyo. Lakini kama ni umuhimu wa kupoteza mvuto siku ya kilele kwa kuwa utambulisho wa wachezaji wapya tayari utakuwa umeonekana kupitia TV, bado zinaweza kufanya jambo kama hilo kwa kuanzia Dar es Salaam na kisha kuchagua kanda mojawapo kwenda kucheza mechi moja kubwa ya kirafiki ambayo itaambatana na burudani zote ili kuwaleta karibu mashabiki wao.

Nipashe tunatamani kuona timu hizo kongwe nchini ambazo zimeteka mashabiki wa soka kila kona, zikiwa chanzo kikubwa cha kivutio cha utalii Tanzania kwa kutumia kila tone la fursa ambalo linaweza kuwa chanzo kikubwa cha mapato lakini pia zikitumika kuutangaza mpira wa Tanzania ndani na nje ya nchi ili kuvutia wawekezaji wakubwa zaidi.

Leo hii tunaona uwekezaji mkubwa katika soka ukiongezeka hadi klabu ndogo kama Singida Big Stars ambayo imepanda Ligi Kuu msimu huu ikiwa na wadhamini kibao jambo ambalo limeifanya kuweza kusajili nyota kibao wa kigeni wakiwamo watano kutoka Brazil.

Tunaamini kupitia Simba na Yanga, ambazo zinajulikana zaidi ndani na nje ya nchi kama ambavyo zinalitangaza soka letu kwa sasa, bado zinaweza kufanya jambo kubwa zaidi kupitia matamasha hayo kwa kuwa chanzo kikubwa cha wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza kwa klabu zetu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# TFF itoe adhabu kali kwa waharibu soka

**HALI** hii inayoonekana sasa kujitokeza, inaweza kuipeleka Tanzania kwenye nyakati mbaya zaidi kisoka, ambazo hazijawahi kushuhudiwa tangu nchi hii ilipopata Uhuru mwaka 1961.

Katika hali ya kushangaza na isiyokuwa ya kawaida, Msemaji wa Yanga aliyesimamishwa kufanya shughuli yoyote ya soka, Haji Manara, aliingia Uwanja wa Benjamin Mkapa na kuchukua kipaza sauti akianza kuwanadi wachezaji wa klabu hiyo, licha ya kwamba ana zuio lililotoka kwenye Kamati ya Maadili kumfungia kufanya shughuli zote za soka kwa kipindi cha miaka miwili na faini ya Sh. milioni 20 juu.

Alifungiwa baada ya kupatikana na kosa la kumtolea maneno yasiyofaa Rais wa TFF, Wallace Karia kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA kati ya Yanga na Coastal Union iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Julai 2, mwaka huu.

Manara aliomba radhi kwa Rais Karia, lakini baadaye akaitisha tena mkutano wa waandishi wa habari na kuongea maneno yaliyoonyesha kuwa huenda alilazimishwa kuomba msamaha na baada ya hapo akaongeza maneno ambayo hayakuwa mazuri sana kwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Siku chache baada ya hapo, akaibuka na kuomba radhi, ingawa ilikuwa kwenye video fupi na si kuita waandishi wa habari kama alivyofanya mwanzo.

Cha ajabu huyo huyo tena akaibuka tena kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, na kuendelea kufanya kazi ile ile ambayo Kamati ya Maadili ilimtaka asifanye.

Huwezi kulitaja tukio hili kuwa ni la aina yake na halijawahi kutokea tangu nchi hii inapata Uhuru kwa mwanachama au mwanafamilia wa soka, kukiuka kile ambacho ameagizwa, au kutotekeleza adhabu iliyotolewa na mamlaka tu, bali ni la kumdhalilisha Rais Karia mwenyewe, TFF, Kamati ya Maadili na Mawakili wake, wadau wa mpira wa miguu na soka lenyewe la Tanzania.

Hivi ninavyoandika ni kwamba kamati hiyo imeshawatia kifungoni wadau mbalimbali wa soka, pamoja na makocha ambao wameendelea kutekeleza agizo hilo, lakini yeye Manara kwa sababu anazozijua mwenyewe amekiuka.

TFF sasa inatakiwa kuamka na kuacha kuchukulia masuala haya kama ni ya kawaida, kwani iwapo ikifumbia macho haitoweza tena kuwa na mamlaka kwenye soka la Tanzania.

Lakini baadaye linaweza kuleta mkanganyiko na vurugu, kiasi kwamba si kwamba itashindwa kusimamia mpira wa miguu, lakini kuiingiza nchi kwenye matatizo na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) na kutokea kama yalivyotokea nchini Kenya ambapo sasa wamefungiwa.

Iache huruma na kumwangalia mtu usoni, badala yake itoe adhabu kali na kuisimamia ili iwe fundisho kwa wote ambao huenda ambao wangeweza kuiga tabia hii ili kulinda na kutetea soka la Tanzania.

Kitu kilichofanywa hapo ni dharau kubwa kwa mamlaka iliyokuwapo na hiyo itakuwa ni mtihani kwao, kwani iwapo itashindwa kutoa adhabu kubwa zaidi ya hapo, kuna wengine watakuja kufanya mbele ya safari TFF itashindwa kutoa adhabu kwa sababu huko nyuma kuna mtu ilimwachia.

Nimeona Sekretarieti imefungua mashtaka kwa tukio hilo na imelipeleka kwenye Kamati ya Maadili, lakini kwa sasa tunatarajia si adhabu tu pekee, lakini pamoja na usimamiaji ili lisijitokeze tena suala kama hili. Mfano Manara angezuiwa kuingia uwanjani haya yote yasingetokea.

Kinachosikitisha kingine ni kwamba pamoja na kwamba kwenye soka kumeingia na watu wasomi tofauti na zamani, lakini wameonekana kutoheshimu mamlaka, sheria na kanuni zilizowekwa.

Huko zamani hakukuwa na wasomi wengi kwenye soka, lakini waliheshimu na kutii maamuzi, sheria na kanuni, cha ajabu kwa sasa kuna ombwe la baadhi ya viongozi na wadau wasomi ambao wanaona kama kwenye soka unaweza kufanya lolote lile bila kufanywa chochote, na mambo ya sheria, kanuni yako kwenye kada zingine na si mpira wa miguu. Hii ni dharau.

Kazi ya TFF sasa kwanza kabisa ni kuanza tena kuusafisha mpira ili urejee kuwa utani, burudani, kuleta umoja, mshikamano na undugu na si uhasama, vurugu, ubabe na kutotii taratibu zilizowekwa.

Vinginevyo kuna siku tunaweza kuona hata mchezaji mwenye kadi nyekundu analazimishwa kucheza mechi kwa kiburi cha 'mtatufanya nini?'




Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Jonas C. Kilima (kushoto), akipokea machapisho yenye taarifa mbalimbali kuhusu Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma WCF, Laura Kunenge, wakati alipotembelea Banda la Mfuko huo kwenye Maonesho ya Nanenane jijini Mbeya. Kulia ni Ofisa Mfawidhi wa WCF, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rose Satta. **PICHA: KHALFAN SAID**

# WCF yaelimisha wakulima, wafugaji mafao

**Na Khalfan Said,** MBEYA

MKURUGENZI wa Huduma za Tathmini, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), amesema maonesho ya Nanenane mwaka huu yana maana kubwa kwa mfuko huo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, alisema kaulimbiu ya maonesho hayo inayosema "Agenda 10/30 Kilimo ni Biashara; Shiriki Kuhesabiwa ili kutekeleza vizuri Mipango ya Kilimo, Ufugaji na Uvuvi" inaakisi moja kwa moja shughuli na mipango ya WCF kwa maana hivi sasa kilimo hiki sio kile cha mazoea kwani kinatarajiwa kuheshimiwa na kuthaminiwa kama ilivyo biashara zingine.

"Serikali imedhamiria kukifanya kilimo chetu kuwa cha biashara na ndiyo maana kaulimbiu inataja kilimo ni biashara, kwa hivyo hapa unazungumzia ajira za wafanyakazi," alisema.

Alisema masuala ya ajira maana yake moja kwa moja WCF inaingia, wote walioajiriwa ni wadau wa Mfuko wa Fidai kwa Wafanyakazi na pindi wanapopatwa na changamoto za ajali au magonjwa yanayotokana na kazi wanapokuwa wanatekeleza shughuli zao za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa namna moja ama nyingine watastahili kulipwa fidia, alisisitiza Dk. Omar.

"WCF tuko hapa kukutana na wakulima, wafugaji na wavuvi ili na wao waweze kujua haki zao mbalimbali ni mafao gani wanaweza wakapata," alisema.

Alisema kama wanavyotekeleza jukumu la kulipa fidia kwa wafanyakazi wanapoumia au kuugua kutokana na kazi kwa mujibu wa mikataba yao ya kazi, pia wakulima, wafugaji na wavuvi watastahili kupata haki za kufaidika na mafao hayo kwa vigezo vile vile vinavyotumika.

Aliyataja mafao hayo kuwa ni pamoja na la matibabu, fidia ya ulemavu wa muda, mafao ya ulemavu wa kudumu na yanaweza kuwa ya mkupuo au kulingana na aina ya ulemavu inaweza kuwa pensheni ya kudumu na endapo itatokea amefariki, wategemezi wake watalipwa fidia na mfuko.

Kuhusu viwango vya uchangiaji katika Mfuko, Dk. Omar alisema hivi sasa serikali imepunguza viwango vya michango kutoka asilimia 0.6 kwenda 0.5 kwa waajiri walio katika sekta binafsi sawa na walio sekta ya umma.

Wakizungumza baada ya kutembelea banda la WCF, wafanyakazi wameipongeza serikali kwa kuuwezesha Mfuko huo ili kuwahudumia wafanyakazi wanapopatwa na tatizo wawapo kazini. "Ni jambo jema sana mfanyakazi anapokuwa anatekeleza majukumu yake na ikatokea amepata changamoto za kuumia, kuugua ama kufariki akiwa kazini aweze kupata haki yake ya kufidiwa ni kitu kizuri na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuuwezesha Mfuko huu kutekeleza majukumu yake," alisema John Chazi, mfanyakazi kwenye Chuo cha Kilimo Inyala, Mbeya.

Naye Aloyce Gonzaga, alisema amekutana na kitu kipya kwa kuwa alikuwa anausikia Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi na aliamua kutembelea banda la WCF ili kupata uelewa zaidi wa namna gani mfanyakazi anaweza kufidiwa endapo atapata madhila yoyote akiwa kazini.

Aidha, Ofisa Mfawidhi wa WCF Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rose Satta, alisema katika maonesho hayo WCF imekuwa ikitoa elimu ya fidia kwa wafanyakazi kwa wananchi wote wanaotembelea banda hilo na kutoa wito kwa wafanyakazi kutoka sekta zote walio katika ajira rasmi kwenye kanda hiyo kutembelea Ofisi za WCF zilizoko jijini Mbeya.

## DC Mpogolo: Royal Tour imeongeza watalii

**Na Mary Geofrey,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupitia kampeni yake ya Royal Tour, iliyoongeza watalii wilayani humo kutoka 300 hadi 6,250 kwa mwaka.

Alisema kwa kipindi cha mwezi mmoja uliopita jumla ya watalii 1,212, walifika wilayani humo jambo ambalo halijawahi kutokea.

Alitoa shukrani hizo mbele ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, mwishoni mwa wiki wakati akiwa wilayani hapo kusitisha ziara yake ya siku tano mkoani Kilimanjaro.

Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi, miradi ya maendeleo na kuhimiza sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

"Naomba utufikishie salamu zetu kwa Rais Samia ametusaidia Wilaya ya Same kupata watalii wa kutosha kupitia kampeni ya Royal Tour. Hatujawahi kupata idadi hii kubwa ya watalii katika wilaya yetu," alisema Mpogolo.

Aidha, alimshukuru Rais Samia kwa kutoa Sh. bilioni 47 kwa ajili ya miradi ya maendeleo wilayani humo.

"Bajeti tuliyotengewa kwa mwaka huu ni kubwa sana Mheshimiwa Katibu Mkuu, awali tulizoea kupata bilioni 10 na zaidi kidogo, lakini sasa tumepokea kiasi hicho kikubwa cha fedha tunaishukuru serikali kwa hili," alisema Mpogolo.

Pia alisema wilaya hiyo inaendelea vyema na maandalizi ya sensa ya watu na makazi itakayofanyika mwezi huu na tayari makarani 1,845 wamepewa elimu kwa kufanya kazi hiyo.

Katibu Mkuu, Chongolo kwa upande wake aliipongeza wilaya hiyo kwa kazi kubwa wanayofanya ya kuwaletea wananchi maendeleo kama ilani ya chama hicho inavyotaka.

# Makada 109 wajitosa ubunge Afrika Mashariki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ZIKIWA zimesalia siku chache kufungwa kwa pazia la uchukuaji fomu za kuomba kuwania ubunge wa Afrika Mashariki kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), hadi sasa makada 109 wamejitosa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Miongoni mwao ni waliowahi kuwa wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wabunge wa Afrika Mashariki.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo, Katibu wa NEC, Oganaizesheni ya CCM, Dk. Maudline Castico, alisema wanachama hao wamejitokeza kuchukua fomu kwenye Makao Makuu ya CCM Dodoma, Ofisi Kuu Zanzibar na Ofisi Ndogo, Dar es Salaam.

"Hadi Agosti 6, mwaka huu waliochukua fomu ni 109 niendelee kutoa wito kwa wana-CCM kuchukua fomu ili kutekeleza ahadi yenu kikatiba ya kugombea," alisema.

Aliwataja wanachama hao kuwa ni Laurence Ngolly, Mona Mangula, Faraja Malaki, Nafue Nyage, Francis Songoro, James Millya, Theddy Patrick, Mhandisi Caroline Lyimo, Hamis Rajabu, Daudi Majinge, Methusela Mbajo, Crescentius Magori, Benedict Kikove, Mhandisi Frank Mejooli na Aloyce Mushi.

Wengine ni Comfort Maugo, Mussa Mgata, Doris Mollel, Julieth Rushuli, Alfred Elia, Alfred Sallwa, Gilbert Bankobeza, Doreen Noni, Deodatus Kinawiro, Shedrack Mashauri, Israel Ilunde, Machano Ali Machano, Rahma M. Ibrahim, Sabra Zubeir Said na Faki Ame Kesi.

Wamo pia, Nasikiwa Berya, Amina Mgeni, Ambwene Kajula, Nasser Nzamba, Prackseda Marmo, Maria Kangoye, Shogo Mlozi, Godfrey Shirima, Dk. Paul Anthony, Henry Bulengera, James Kasurura, Alfa Munyi, Manase Michael, Ayubu Lemilya, Nicksoni Kahimba na Mhandisi Haji Vuai Ussi.

Wanachama wengine ni Brigedia Jenerali mstaafu, Marianus Mhagama, Mwanamanga Mwanduga, Conrad Lushakuzi, Balozi Anastase Rwegayura, Khadija Kayanda, Elibahati Lowassa, Masengwa Busigosolwe, Thomas Kitima, Reginald Shirima, Luvuva Salum Ali, Dk. Abdallah Hasnuu Makame na Mmanga Mjengo Mjawiri.

Pia Jonas Lufungulo, Dk. Linda Salekwa, Loti Lembrice, Richard Mbuguni, Angela Kiza, Wakili Msomi Pascal Mayala, Francis Nanai, Melinda Muganda, Fikiri Luganga, Mkondo Fabian, Albert Mbago, Robison Etuttu na David Mwakanjuki.

Pia Amani Kajuna, Azizi Mussa, Judith Mollel, Amedeus Mzee, Kalunde Malale na William Reuben, Fancy Khuni, Salma Mwassa, Ngwaru Maghembe, Happyness Lugiko, Shabu Makonyola, Salimu Kungulilo.

Vilevile, Prof. Norman Sigalla, Harrison Lukosi, Rehema Hassan, Ahmed Nkhuli, Steven Mkomwa, Dorica Gwilenza na Ansar Kachabwa, Nadra Juma Mohamed, Ahmed Shehe Saleh, Mar-yam Said Mussa na Mourie Oscar Sendera.

Majina mengine yaliyotajwa ni Suzana Kabula, Itikija Mwanga, Neema Mwinge, Getrude Haule, Lwitiko Anyingyisye, Salum Kanyungu, Edna Mafuwe, Dk. Salvatory Mhando, Godfrey Simbeye, Elias Komba, Consolata Mulalo, Linus Linda, Lathifa Sykes, Dk. Hamad Khamis Juma na Fatma Ali Omar.

Katibu alisema mwisho wa uchukuaji fomu ni Jumatano ya Agosti 10, mwaka huu.

# Wakulima wafunguka kupata mavuno hafifu

**Na Happy Severine,** BARIADI

BAADHI ya wakulima mkoani Simiyu wamekiri kukosea maelekezo ya utumiaji na uchanganyaji wa sumu ya kuua wadudu na kusababisha kupata mavuno kidogo na yasiyo na tija.

Wamesema miaka mingi walikuwa hawazingatii njia sahihi ya upuliziaji wa sumu ya kuua wadudu na kuelekeza malalamiko mengi kwa Bodi ya Pamba kuwa dawa zao ni bandia na haziui wadudu wakati sio kweli.

Wananchi hao walisema hayo jana wakati wakizungumza na wataalamu wa bodi hiyo walipotembelea banda lao kwenye Maonesho ya Nanenane Kanda ya Ziwa Mashariki yanayoendelea katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Samwel Maduhu, mkazi wa Wilaya ya Itilima, alishukuru bodi hiyo kwa elimu wanayoendelea kuitoa kwa wananchi kwa kuwa wengi wao hawajui namna sahihi ya kutumia sumu za kuua vimelea na wadudu waharibifu wa zao hilo.

Alisema binafsi yeye alikuwa akichanganya tofauti sumu hizo na hata upuliziaji wake ulikuwa ni tofauti na unaoelekezwa na wataalamu wa kilimo na bodi. Kwa upande wake, Jisenda Maduhu alisema kupitia elimu waliyoipata na namna ya kuzingatia na kutumia teknolojia bora za kilimo pamoja na matumizi sahihi ya sumu za kuua wadudu shambani, anaamini msimu ujao atazalisha mazao mengi.

"Nimejifunza vitu vingi kuhusu teknolojia bora za kilimo na vifaa vya kurahisisha kazi za kilimo shambani...nimejua namna sahihi ya uchanganyaji wa sumu ya kuua wadudu shambani...naamini msimu ujao nitazalisha kwa tija," alisema Maduhu.

Aliiomba Bodi ya Pamba kuwaletea majembe ya kupalilia pamba ili kurahisisha kazi hiyo kwani kwa sasa hayapatikani.

Kwa upande wake, Ofisa Kilimo wa Bodi ya Pamba, Said Itaso, alisema kuna mikakati ya kuongeza tija katika zao hilo kupitia teknolojia mbalimbali.

Itaso alisema bodi hiyo itahakikisha kila mkulima anatumia teknolojia bora, kibao cha kupandia na matumizi bora ya sumu za kuua wadudu.



Mkufunzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kipunguni Dar es Salaam Tausi Msangi (aliyechuchumaa), akitoa elimu ya jinsi ya kutengeneza mkaa mbadala kwa kutumikia takataka mbalimbali, kwa wanawake wajasiriamali wa Mikocheni B, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaona umuhimu ukarabati Chuo cha Afya Kibaha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Charles Msonde, amesema kuna haja ya kufanya ukarabati katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Kibaha na kuongeza majengo ili kukidhi mahitaji ya walengwa.

Pia, amesema Ofisi ya TAMISEMI itahakikisha majengo ya kisasa yanajengwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi wanaosoma katika chuo hicho na wakufunzi kutoa huduma katika sehemu nzuri.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa katika mahafali ya wahitimu wa kata ya afya kozi ya Tabibu, Uuguzi na Ukunga.

Alitoa wito kwa wadau wa elimu kusaidia kutatua vikwazo vilivyoko katika chuo hicho na kuwawezesha wanafunzi kupata elimu katika mazingira mazuri.

Kadhalika, Dk. Msonde alisema yapo mazungumzo yanaendelea kuwezesha wanafunzi wa vyuo vya kati waweze kunufaika na mikopo na serikali inaendelea kushughulikia.

"Serikali ilishaweka namna bora ya kuhakikisha ambao hawana uwezo wa kulipa ada, halmashauri zote zilishapewa maelekezo ya kuhakikisha kama maombi yatafikishwa na mtu mwenye uhitaji akachunguzwa ikathibitishwa kweli hana uwezo halmashauri itamlipia ada," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Tusekile Solile, alisema Shirika la Elimu Kibaha, limetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 100 kwa ajili ya upanuzi wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi.

Alisema eneo hilo ni kwa ajili ya ujenzi wa kampasi mpya itakayokuwa na uwezo wa kudahili wanachuo 1000 kwa mwaka.

Dk. Solile alibainisha vikwazo vya chuo hicho kuwa ni pamoja na uhaba wa miundombinu unaosababisha kushindwa kuanzisha kozi mpya za stashahada ya famasia na maabara ya uchunguzi.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa chuo idadi ya vyumba vya maabara hailingani na wanachuo waliopo, uhaba wa miundombinu ambao umesababisha idadi ndogo ya wahitimu wa shule za sekondari kushindwa kupata nafasi ya kujiunga na chuo hicho.

Majengo hayo yanaelezwa kuwa machakavu zaidi kutokana na kujengwa miaka 56 iliyopota, pia miundombinu ya mabomba ya majisafi na majitaka, kuhitaji ukarabati.

# CCM yashauriwa kuadhibu wanao haribu uchaguzi

**Na Sabato Kasika**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeshauriwa kuwachukulia hatua za kinidhamu viongozi wake wa ngazi waliohusika kuvuruga uchaguzi unaoendelea ndani ya chama hicho kwenye baadhi ya maeneo nchini.

Ushauri huo umetolewa na kada wa chama hicho, Thomas Ngawaiya alipozungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana, kuelezea kasoro zinazoendelea kujitokeza katika uchaguzi wa ndani ya chama hicho.

"Kama unafuatilia uchaguzi ndani ya chama chetu, kumekuwapo na kasoro zinazofanywa kwa makusudi na baadhi ya viongozi ili kuweka watu wao, hali ambayo inaweza kudumaza demokrasia ndani ya chama," alisema Ngawaiya.

Alifafanua kuwa Aprili mwaka huu, kasoro zilijitokeza katika uchaguzi wa ngazi ya mashina na matawi na kusababisha Katibu Mkuu wa chama, Daniel Chongolo kuagiza uchukuaji fomu urudiwe upya.

"Tumesikia mengine huko Mwanza kuwa rafu zimefuta kufutwa. Kwa hali kama hii, ninashauri viongozi wanaosababisha haya wachukuliwe hatua za kinidhamu ikiwamo kupewa onyo, kusimamishwa uanachama au kufukuzwa kulingana na ukubwa wa kosa, wanakidhalilisha chama," alisema.

Alisema viongozi wanaosimamia uchaguzi ndani ya chama wanatakiwa kuacha chaguo la wapigakura litawale, kwa kuwa wao ndiyo wanaowajua wanaotaka wawaongoze.

"Chama kina kanuni na taratibu zake za uchaguzi ambazo ni lazima zifuatwe sio kuzipindisha na kupitisha wagombea bila kupingwa au watu kutumia majina ya viongozi wa chama kutaka nafasi," alisisitiza.

Ngawaiya ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), alisema CCM ni chama kikongwe kinachozingatia demokrasia na kwamba kisuruhusu baadhi ya watu kukiharibia sifa hiyo.

"Sisi taasisi ya utawala bora tunaamini kwamba viongozi bora wanapatikana kwa njia halali, bora viongozi wanapatikana na mbinu chafu kama hizo ambazo zimesababisha baadhi ya uchaguzi kufutwa," alisema.

Alifafanua kuwa hata upigaji wa kura za maoni unatakiwa kuzingatia mshindi wa kura hizo badala ya kupitisha aliyeshika namba mbili au juu hiyo, kwa madai lisipozingatiwa linasababisha kuchaguliwa viongozi wasiofaa ama kuzusha sintofahamu miongoni mwa wanachama.

Aprili mwaka huu, Katibu Mkuu wa CCM Daniel Chongolo, aliwaagiza makatibu wa chama hicho ngazi ya wilaya kurudia mchakato wa utoaji fomu kwa wagombea wote ngazi ya mashina baada ya kubaini baadhi ya wanachama kunyimwa fursa hiyo kwa makusudi.

Alitaja baadhi ya maeneo yaliyokumbwa na figisu hizo, katika uchaguzi kuwa ni Tandika Kimara na Manzese mkoani Dar es Salaam, kwa baadhi ya makatibu wa matawi kuwanyima fomu wagombea kwa maslahi yao binafsi.

Chama hicho kimemaliza uchaguzi wa viongozi wa jumuiya zake za UWT, wazazi na vijana katika ngazi ya kata, na leo kinatarajia kuendelea na uchaguzi wa viongozi wa chama katika ngazi hiyo.

HABARI KITAIFA

## Wanafunzi kufundishwa kujikinga maambukizi VVU

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHULE 135 za msingi na sekondari Halmashauri ya Wilaya ya Singida zimepatiwa vishikwambi vitakavyotumika kuwafundisha wanafunzi masuala ya elimu ya uzazi na jinsi ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Ester Chaula, akizungumza juzi wakati wa ugawaji wa vishikwambi hivyo kwa walimu 270 waliopewa mafunzo ya namna ya kuvitumia, alisema halmashauri yake imekuwa miongoni mwa 20 kati ya 184 zilizogawiwa vishikwambi hivyo.

Alisema serikali imetoa vishikwambi hivyo ili kutoa elimu ya uzazi wa mpango na maambukizi ya VVU ili kufikia malengo ya mradi unaojulikana kama Timiza Malengo unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Chaula alitoa wito kwa walimu pamoja na kwamba vishikwambi vimetolewa kwa ajili ya kufundishia masuala ya elimu ya uzazi, lakini vitaweza kutumika kufundisha masomo mengine kutokana na uwezo wa kuhifadhi 'materials' ya masomo mengine yanayofindishwa shuleni.

Alisema mwelekeo wa serikali ni kufanya kila kitu kufanyika kwa njia ya kidigitali na kutumia teknolojia hiyo kutapunguza matumizi ya karatasi na wanafunzi watafundishwa elimu ya uzazi na jinsi ya kujikinga na maambukizi ya VVU kwa njia ya picha.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mragili, alisema kutolewa vishikwambi hivi ikiwa ni mpango wa serikali wa kutaka kuhama katika utendaji wa analogi na kwenda kwenye utendaji wa kidigitali.

"Tunakokwenda ni kwamba utendaji wote wa serikali kuanzia ngazi ya chini hadi juu utakuwa katika mfumo wa kidigitali, hivyo shule zijipange kuingia katika mfumo huu wa kufundishi kidigitali," alisema.

Mragili alisema shule ambazo zimebahatika kupata vishikwambi hivyo ziwe mfano kutumia vifaa hivyo ili kuzivutia zingine kutumia teknolojia hiyo na shule zione umuhimu wa kuongeza vishikwambi zaidi kwani viwili ambavyo vimetolewa kwa kila shule havitoshelezi.

Alisema walimu lazima watambue kuwa mpango huo ulipoanzisha tayari utafiti ulifanyika na kuona kuna tatizo la elimu ya uzazi kwa vijana hivyo wahakikishe wanafundishwa ili waweze kujitambua na kupunguza maambukizi ya VVU.

"Naomba Singida tuwe miongoni mwa halmashauri zitakazofanya vizuri katika programu hii ili kuwafanya vijana wawe na afya njema na wafikie ndoto zao katika maisha yao," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alisisitiza suala la utunzaji wa vishikwambi hivyo ili visaidie vijana wengine zaidi na kwamba kuvifanya kuwa mali ya shule sio kwamba utunzaji uwe wa kulegalega.

Aidha, aliishukru serikali kwa kutoa vishikwambi kwa kutoonyesha ubaguzi ambapo vimetolewa kwa shule za serikali na binafsi kwa suala la elimu ya afya huwezi kubagua kati ya wanafunzi wanaosoma shule binafsi na za serikali.

# Madiwani walalamika wajawazito kutozwa fedha

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia baadhi ya wajawazito wanaokwenda kujifungua kwa operesheni katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama, kutozwa Sh. 150,000.

Wamesema kitendo hicho kimesababisha wasio na uwezo kujifungulia nyumbani au kwa waganga wa jadi.

Hayo yalibainishwa jana katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Manispaa hiyo cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2021/2022, ambacho kilijadili masuala mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya afya, maji, elimu na barabara.

Diwani wa Viti Maalumu Kata ya Nyahanga, Helena Samson, alisema gharama kubwa za kujifungua, zimesababisha kuwapo malalamiko mengi yakiwamo utozwaji wa Sh. 5,000 kwa ajili ya kitanda na kadi ya kliniki.

"Wakati wa kujifungua wajawazito wanalazimishwa kununua vifaa vipya ya kujifungulia yakiwamo mabeseni mapya, mipira na vitenge na ikibainika una vitenge ambavyo vimetumika wanagoma kukupokea na badala yake wajawazito wanalazimika kwenda kujifungulia majumbani," alisema. Diwani huyo alishauri ili kuondokana na tatizo hilo ni vyema uongozi wa hospitali uweke bango linaloonyesha vitu anavyopaswa mjamzito kwenda navyo wakati wa kujifungua na kama litashindikana watoe mbadala utakaowasaidia wanawake.

Diwani Mkola Athumani, alisema suala hilo tayari walishamweleza Mkurugenzi ili kulishughulikia kwa sababu vinawafanya wananchi kuendelea kulalamika kwa kukosa huduma stahiki hospitalini. Alipendekeza watumishi wa idara ya afya kuwa na nembo kwenye sare zao za kazi zitakazosaidia kuwabaini wanaojihusisha na vitendo vya rushwa kwa wagonjwa.

Mbunge wa Kahama, Jumanne Kishimba alisema idara ya afya imekuwa tatizo kubwa na haitendi haki kwa wagonjwa wenye uwezo mdogo hususani wajawazito ambao wanalazimika kwenda na vifaa vipya vya kujifungulia.

"Suala la ujauzito tunaomba lisiwe kero kwa mjamzito, mabango yenye kuonyesha vifaa gani mjamzito anatakiwa kuwa navyo itakuwa suluhu kwa vitendo vya rushwa vinavyolalamikiwa hospitali," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa, Clemence Mkusa, alimwagiza Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Josephat Shani kuhakikisha suala hilo analitekeleza kwa haraka ili kuondoa malalamiko kwa wagonjwa wanaokwenda hospitalini kupata huduma.

Mganga wa hospitali hiyo, alipokea agizo hilo na kukanusha taarifa za rushwa na kwamba ofisi yake haijapokea malalamiko yoyote kutoka kwa wajawazito kutozwa fedha za kadi ya kiliniki, vitanda au nguo mpya kwa ajili ya kujifungulia.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Orca Energy ambayo ni kampuni mama ya PanAfrican Energy, Jay Lyons, wakati wa kongamano la Nishati Tanzania 2022 lililofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Waeleza chanzo watoto kutumikishwa machimboni

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANANCHI wanaoishi maeneo ya machimbo ya madini ya almasi wilayani Kishapu, mkoani Shinyanga, wametaja sababu za watoto kuendelea kutumikishwa kwenye machimbo hayo kuwa ni wazazi kuwatekeleza na kuamua kujitafutia maisha yao wenyewe.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na mjumbe wa Kamati ya Mpango mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), Magrett Ngeleja, Kijiji cha Songwa wilayani Kishapu, kwenye ufungaji wa mafunzo ya kujengewa uwezo kamati 11 katika vijiji vinavyozunguka mgodi wa Mwadui. Alisema tatizo la watoto kutumikishwa kwenye machimbo ya madini, linatokana na wazazi wao kuzitekeleza familia na watoto kuamua kujitafutia riziki maeneo ya migodini ili waweze kuendesha maisha yao.

"Ukatili kwenye maeneo ya machimbo ya madini upo mkubwa sana hususani kwa wanawake na watoto, hivyo kupitia elimu ambayo tumeipata tutakwenda kutoa elimu kwa jamii kuachana na vitendo vya ukatili na kuzitunza familia zao," alisema Ngeleja.

Naye mwezeshaji wa mafunzo hayo, Rose Shao, alisema alichokibaini kwenye maeneo mengi ambayo yana machimbo ya madini kuna ukatili kwa wanawake na watoto, na kuitaka jamii maeneo hayo zibadilike na kuishi salama.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya HER DIGNITY, Annagrace Rwehumbiza, alisema wamekutana na kamati za MTAKUWWA katika vijiji 11 vilivyoko katika machimbo ya madini Mwadui ili kutoa elimu na kujadiliana namna ya kupunguza ukatili au kuumaliza katika maeneo hayo.

# RITA yatoa vyeti vya kuzaliwa Nanenane

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), umesajili na kutoa vyeti vya kuzaliwa kwa wakulima pamoja na wananchi wote waliozaliwa ndani ya mipaka ya Tanzania Bara.

Akiongea kutoka katika viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya, Ofisa Usajili kutoka RITA, Noela Ituga, alisema kuwa wakulima lazima watambue umuhimu wa cheti cha kuzaliwa na kuwa nacho mapema kwa matumizi mbalimbali katika jamii ikiwamo kupata pasi ya kusafiria ili kuweza kusafirisha mazao nje ya Tanzania na kukuza soko la mazao ya biashara nchini.

Akizungumzia faida za cheti cha kuzaliwa, Ituga alisema: "Ijapokuwa haya ni maadhimisho ya siku ya wakulima, lakini pia RITA imewaletea huduma ya kusajili cheti cha kuzaliwa kwa kila mwananchi aliyezaliwa Tanzania Bara kwani mbali na kuwa cheti hicho kinatambulisha ubini wa mtu, lakini kinatumika katika kupata pasi ya kusafiria, kitambulisho cha uraia, ajira, bima ya afya, mikopo ya elimu ya juu pamoja na kuzuia ajira za utotoni.

Hivyo basi, tunapenda kuwasihi wakulima pamoja wananchi wote kwa ujumla kufika katika banda letu ili kusajili cheti hicho pamoja na kupata elimu kwa umma kuhusu usajili wa ndoa na talaka, huduma ya ufilisi, udhamini pamoja na msaada wa kisheria kuhusu wosia na mirathi."

RITA inashiriki katika sherehe za maadhimisho hayo yanayofanyika kitaifa mkoani hapa.

# Wakumbushwa uzingatiaji sheria ufugaji soko la maziwa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

KAMPUNI ya wazalishaji maziwa iliyoko Kingolwira Magereza Manispaa ya Morogoro, imewataka wafugaji wa nje kuongeza uzalishaji na kusimamia sheria na kanuni za ufugaji zilizoko ili kampuni ikidhi mahitaji ya kuzalisha lita 1,000 kwa siku badala ya lita 20 inayozalisha kwa sasa.

Mkaguzi Msaidizi wa Magereza, Samson Kitundu, alisema hayo jana kwenye banda la maonesho ya 46 ya Sikukuu ya Wakulima 88, Kanda ya Mashariki yanayofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, yanayohusisha mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro na Tanga na kampuni hiyo baada ya kuona kuwa inakabiliwa na upungufu wa maziwa kwa ajili ya uzalishaji wameamua kununua kutoka nje na kuwanufaisha wafugaji wengine.

Kitundu alisema awali walianza kusambaza maziwa freshi kwa wateja Manispaa ya Morogoro na baadaye kuona haja ya kuyaongezea thamani na kutengeneza mtindi.

Alisema walitegemea maziwa kutoka kwenye shamba lao, lakini wanatarajia kununua pia uraiani kutokana na kiwanda chao kuwa na uwezo wa kuzalisha kwa siku lita 1,000 huku kwa sasa wakizalisha lita 20 na tayari wameshapata nembo ya ubora ya TBS.

Alisema wanasambaza maziwa katika masoko ya mikoa mbalimbali ikiwamo Morogoro, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam na bei zake ni za chini zaidi na ubora na ladha tofauti zaidi inayowafanya wateja kurudia mara kwa mara kuyanunua.

Aliwataka watumiaji maziwa kutumia hasa mtindi kutoka Kingolwira ambayo yanatengenezwa vizuri kiasili na kurahisisha mmeng'enyo.

Alisema katika kuzalisha ajira kwa majirani zao, wanajipanga kutoa elimu kwa wafugaji na kuwaelimisha mbinu za ufugaji ili kupata maziwa bora.

Alisema elimu hiyo itasaidia wafugaji kupata maziwa yenye uzito, joto zuri, yasiyo na magonjwa na dawa zinazotokana na sindano anazochomwa ng'ombe mambo ambayo yatathibitishwa kupitia vipimo mbalimbali.

Pia watalazimika kupokea maziwa bora ambayo hayana tatizo lolote kwa binadamu kama wanayoandaa wao ili mfugaji aweze kupata faida na wao wanayaongezea ubora na kupata faida.

Alisisitiza Watanzania kuzingatia unywaji maziwa kutoka Tanzania badala ya vitu vya nje ya nchi kwa kuwa ni kitu cha msingi kwenye afya ya mwanadamu na kuwaepusha na magonjwa ikiwamo kifua kikuu na kwamba maziwa mtindi ni protini yenye faida kwa jamii hasa kwa wanaume kwenye tendo la ndoa.

Naye mmoja wa wafugaji, Richard Mwendo, alipongeza uanzishwaji wa kiwanda hicho Manispaa ya Morogoro ambacho alisema kitakuwa mkombozi kwao katika kupata soko la maziwa wanayozalisha kutoka kwenye mifugo yao.



Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dietram Mkapa (kushoto), akitoa maelezo kwa wakulima kuhusu mkungu wa Fhia maarufu ndizi Bukoba wenye kilo zaidi ya 100. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Mikungu ya ndizi inayozaa kilo 100 yawa kivutio

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

MIKUNGU ya ndizi aina ya Fhia (ndizi Bukoba) yenye kilo zaidi ya 100 imekuwa kivutio kwa wakulima na wananchi kutoka mikoa mbalimbali nchini kufurika kwenye banda la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kwenye Maonesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa mkoani hapo.

Akizungumzia teknolojia hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema imefanyiwa utafiti na maboresho katika kituo cha TARI- Maruku mkoani Kagera kwa kuchanganywa kutoka aina za mbegu ya kienyeji wanazotumia wakulima nchini.

Dk. Mkamilo, alisema utafiti wa mbegu hizo bora za migomba umechukua miaka 18 na sasa wapo katika hatua ya kusambaza kwenye mikoa inayolima zao hilo ikiwamo Mkoa wa Kagera, maeneo ya Ukanda wa Ziwa ikiwamo Mkoa wa Mara, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya na Morogoro.

Alisema kutokana na TARI kuwa na jukumu la kufanya utafiti na kusambaza teknolojia ya mbegu bora kwa wakulima, katika maonesho hayo wamekuja na mbegu za migomba ikiwamo aina Taribani 1 mpaka Taribani 4 ambazo zinazaa kuanzia tani 20 mpaka tani 70 kwa hekta kwa mwaka.

"Hizi mbegu bora za migomba tulizofanyia utafiti katika kituo chetu cha TARI-Maruku zinazaa tani 70 mpaka 100 kwa hekta kwa mwaka tofauti na tani 10 mkulima anazopata kwa kutumia mbegu zake za kienyeji ndiyo maana tumezileta hapa ili kuwapa elimu wakulima watumie hiyo mbegu," alisema Dk. Mkamilo.

Mikungu hiyo ya ndizi iliyokuwa kivutio katika maonesho hayo na kushangaza wakulima kutokana na kuwa na zaidi ya kilo 100 ni moja ya mbegu bora zilizofanyiwa utafiti na kuleta tija kubwa pamoja na kuwa na ukinzani wa magonjwa ya migomba kama mnyaukofuzali, sikitoka na wadudu wa zao hilo.

Mkurugenzi wa TARI-Maruku, Dk. Mpoki Shimwela, alisema pamoja na kufanya utafiti huo na kuja mbegu bora za Taribani 1 mpaka 4 na Fhia 23, Fhia 27, na 17, wameamua kuzihamasisha aina ya mbegu Fhia ambazo pia zimezoeleka kwa jina la ndizi Bukoba au matoke kutokana na uzaaji wake mkubwa na kuhimili ukame.

"Hizi ndizi katika hali ya kibiashara ni moja ya ukombozi mkubwa kwa wakulima hapa nchini kwa kuwa zinastahimili sana magonjwa na hali ya ukame na hivyo kumpa mkulima kipato kwa kuwa uzaaji wake ni mikungu mikubwa zaidi ya kilo 100 hivyo kuleta hamasa ya kibiashara," alisema Dk. Shimwela.

Alisema, wakulima wanapaswa kujivunia mbegu hizo zilizovumbuliwa nchini na mkakati ulioko ni kueneza mikoa yote inayolima ndizi na tayari wameshaanzisha mashamba darasa katika Taasisi za TARI kwenye mikoa ya Morogoro, Arusha, Bukoba na Mbeya ambazo mbegu hizo zinapatikana.

John Mwalusamba mmoja wa wakulima kutoka mkoani Mbeya aliyetembelea banda hilo kujionea teknolojia hiyo mpya ya mbegu ya migomba, alipongeza TARI kwa kuleta ukombozi kwa wakulima kutokana na baadhi ya mbegu zimekuwa zikishambuliwa na wadudu.

Nipashe
Spotika



SAJILI 5 BORA ZAIDI ZA THAMANI YA FEDHA UK. 12-13







# WACHEZAJI WA5 WENYE UJUZI ZAIDI DUNIANI KWA SASA 2022

**LONDON,** England

BILA kujali muktadha wa mchezo, mashabiki wa soka daima watashangilia onyesho la ustadi na ufundi dimbani. Mbali na kuwa wanasoka wa ajabu, ni ujuzi wao wa hali ya juu wa kucheza na mpira ambao umewafanya watu kama Ronaldinho na Ronaldo Nazario kupendwa na dunia.

Inafurahisha kuwatazama wanasoka wakiwazidi ujanja wapinzani wao kwa hila na mbwembwe zao. Sio tu dalili ya jinsi ufundi wa mwanasoka ulivyo mzuri, lakini ni onyesho la uwezo wake wa kufikiria hatua moja mbele ya adui yake.

Baada ya yote, kumfanya mpinzani akisie na kutowahi kumjulisha hatua yake inayofuata ni muhimu ili kupata mafanikio kwenye uwanja wa mpira.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano waliobobea katika mbinu na ujuzi wa soka la dunia kwa sasa...

**#5. Vinicius Jr (Real Madrid)**

Hadi mwanzoni mwa msimu wa 2021-22, Vinicius Jr. alionekana kama winga mwenye busara aliyebarikiwa na ustadi mwingi. Lakini jambo kuhusu wachezaji kama Vinicius ni kwamba, wanapofanya mabadiliko katika upande wa kiufundi wa mambo, huwa hawawezi kuzuilika.

Winga huyo wa Brazil aliboresha uchezaji wake wa kumalizia na wa kiungo kwa njia kubwa muhula uliopita. Alifunga mabao 22 na kutoa asisti 20 katika mechi 52 kwenye mashindano yote akiwa na Real Madrid msimu wa 2021-22.

Lakini kinachomfanya Vinicius kuwa pendekezo la kutisha kwa mabeki ni uwezo wake wa kudhibiti mpira na kucheza chenga. Kiwango chake cha chini cha uvutano humwezesha kutekeleza kiajabu na kila mara huwafanya mabeki wakisie na hushindwa kumdhibiti.

**#4. Lionel Messi (Paris Saint-Germain)**

Lionel Messi ni mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote. Kitu cha kipekee kuhusu Messi tofauti na wachezaji wengine kwenye orodha hii ni kwamba, yeye si mtu wa kufanya ujanja wa ajabu. Mshindi wa rekodi ya Ballon d'Or mara saba anatumia udhibiti wake wa karibu, kushuka kwa bega na kuzunguka kwa nyonga ili kuwashinda wapinzani wake.

Messi huwa anahamisha tu mpira kutoka mguu mmoja hadi mwingine ili kukwepa changamoto kabla ya kumpita beki anayekimbia kwa kasi kuja kwake.

**#3. Ousmane Dembele (Barcelona)**

Kuna wanasoka wachache duniani ambao wanaweza kupiga shuti vema kwa mguu wowote. Lakini kuna wachezaji wachache sana ambao wanaweza kupiga chenga vizuri kwa miguu yote miwili. Ousmane Dembele ni moja ya matukio kama haya.

Yeye ni winga mwepesi sana na mjanja ambaye kufanya maamuzi na uelekevu ndani ya tatu ya mwisho kunamfanya kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye mchezo. Hivi majuzi Dembele aliitia hofu Juventus katika mechi ya kirafiki ya kujiandaa na msimu mpya kwa ustadi wake wa kuchezea mpira, akifunga mabao mawili ya kuvutia.

Ustadi wake umejaa chenga za ghafla, kuzungusha na kwa urahisi ni mmoja wa wachezaji wanaosisimua zaidi kuwatazama kwenye mchezo kwa sasa.

**#2. Allan Saint-Maximin (Newcastle United)**

Uwezo wa Allan Saint-Maximin akiwa na mpira miguuni mwake ni wa ajabu. Uvumbuzi wake wakati wa kusonga mbele na kuwachambua mabeki ni jambo la kufurahisha kutazama na kumfanya kuwa mshambuliaji namba moja wa Newcastle United katika safu ya ushambuliaji.

Kwa bahati mbaya, mchezaji huyo Mfaransa bado thamani yake hailingani na ujuzi wake. Hata wakati wa siku za kocha Steve Bruce, hakuwa na nafasi kubwa.

Lakini chini ya Eddie Howe, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 anatarajiwa kupeleka mchezo wake katika ngazi nyingine. Kwa hakika ana uwezo na ikiwa anaweza kuboresha mchezo wake kwa ujumla, anaweza kuwa mshindi wa dunia.

**#1. Neymar Jr (Paris Saint-Germain)**


Neymar ni mchezaji anayefanana na magwiji wa Brazil kama Ronaldinho na Ronaldo Nazario, ambao walijulikana kwa ustadi wao wa 'samba' na muunganisho maalum wa mpira. Winga huyo wa Paris Saint-Germain ni kitu cha kutazamwa kila anapopata mpira.

Neymar Jr ni jasiri sana hata anatekeleza kwa mafanikio mbinu za mazoezi kama vile upinde wa mvua wakati wa michezo halisi ya ushindani. Inahitajika kujiamini sana katika uwezo wa mtu ili kuvuta ujuzi kama huo katika kiwango cha juu zaidi cha mchezo.

Yeye ni mmoja wa washambuliaji bora wa zama za kisasa na bila shaka ndiye mwanasoka mwenye ujuzi zaidi duniani kwa sasa.

## ISIKUPITE

NAHODHA wa AFC Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 23, wa Arsenal, Martin Odegaard (23) na wa West Ham United, Declan Rice (23), ndio manahodha wenye umri mdogo zaidi hadi sasa kwenye Ligi Kuu England msimu huu.



# SAJILI 5 BORA ZAIDI ZA THAMANI YA FEDHA


KOULIBALY

**LONDON,** England

BADO kuna safari ndefu katika soko la usajili la msimu wa joto wa 2022 na klabu zinaweza kuhitimisha mikataba mingine mikubwa zaidi. Erling Haaland, Darwin Nunez, Robert Lewandowski, na wengine kadhaa tayari wametia muhuri na wameingia vema katika klabu zao mpya.

**Lakini nyuma ya pazia, klabu chache zimeweza kusajili wachezaji wa kiwango cha juu kwa ada ndogo. Aidha, pande hizi zimetumia vema hali ya kimkataba ya mchezaji au kuwapa nafasi kubwa katika timu.**

Kwa kuzingatia hilo, hebu tuangalie sajili tano bora zaidi za thamani ya fedha kubwa kwa Julai 2022.

Kumbuka: Takwimu zote hazijumuishi wachezaji waliosajili kwa uhamisho wa bure, twende sasa...

### #5. YVES BISSOUMA KWENDA TOTTENHAM HOTSPUR - PAUNI MILIONI 25

Tottenham Hotspur hatimaye wamemuunga mkono kocha wao kwa kutumia fedha nyingi kwenye soko la usajili msimu huu wa majira ya joto. Antonio Conte bila shaka ndiye mtu wao muhimu zaidi wa kumaliza ukame wao wa takriban miaka 15 bila taji, kwa hiyo haishangazi kwamba, klabu imefanya usajili ubora.

Ivan Perisic na Fraser Forster waliwasili bila malipo huku Richarlison na Djed Spence wakijiunga kwa pauni milioni 50 na pauni milioni 12.5. Clement Lenglet pia amesajiliwa kwa klabu hiyo kwa uhamisho wa mkopo kutoka Barcelona.

Biashara yao bora zaidi, hata hivyo, ni ununuzi wa nyota wa zamani wa Brighton & Hove Albion, Yves Bissouma.

Bissouma ambaye ni mjuzi kabisa katika safu ya kiungo, tayari ana uzoefu wa miaka minne kwenye Ligi Kuu England. Licha ya hayo, alifikisha umri wa miaka 25 tu Aprili mwaka huu na bado ana miaka yake bora mbele yake. Chini ya Graham Potter, mchezaji huyo wa kimataifa wa Mali aliendeleza ubora wake.

Spurs wamekuwa wakimlilia mchezaji wa hadhi yake tangu kuondoka kwa Moussa Dembele mwaka 2019. Huku Pierre Emile Hojbjerg na Rodrigo Bentancur wakiwa viungo pekee wenye uzoefu katika kikosi, Bissouma anakaribishwa.

Harry Winks anaripotiwa kuwa nje ya mipango ya Conte msimu huu huku Oliver Skipp akiwa bado hajajidhihirisha kabisa katika kiwango cha juu.

Hivyo, kujaza nafasi hiyo muhimu uwanjani kwa kusajili mchezaji wa kiwango cha nyota huyo wa Kiafrika kwa pauni milioni 25 tu (iliyopanda hadi pauni milioni 35) ilikuwa ni hatua ya busara. Bei iliyopunguzwa inahusiana na Bissouma kuwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake na Brighton.

### #4. SADIO MANE KWENDA BAYERN MUNICH- PAUNI MILIONI 26

Kama Bissouma, Sadio Mane pia aliingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Liverpool msimu huu wa majira ya joto. Kwa hiyo, ilimjia kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake na Msenegal huyo aliamua kuanza maisha mapya.

Bayern Munich iliona hii kama fursa ya kuitumia vema kwa kusajili mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani (kwa sasa). Liverpool hawakuwa na tatizo la kumwachia Mane, mradi tu bei yao ya pauni milioni 26 ilifikiwa na klabu hiyo ya Ujerumani.

Hata hivyo, timu hiyo ya Bundesliga itahisi kwamba imepata thamani kubwa kabisa. Ingawa mara nyingi alifunikwa na Mohamed Salah.

Takwimu zake pia si mbaya sana kwani alifunga mabao 120 na kutoa asisti 48 katika mechi 269 kwenye mashindano yote kwa 'Wekundu' hao.

Katika kipindi hiki, alishinda kila kombe la ndani, pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya, mashindano ambayo alihusika katika mabao 32 kwenye michezo 55 pekee. Baada ya kuondoka kwa Robert Lewandowski msimu huu wa majira ya joto, kuwasili kwa Mane si tu nyongeza nzuri kwenye kikosi, lakini pia ni wakati muafaka.

Bayern watahitaji mtu wa kuchukua nafasi ya idadi kubwa ya mabao ya nyota wao wa Poland aliyeondoka na akiwa na umri wa miaka 30, Mane bado ana mengi ya kufanya. Kwa hiyo, kulipa tu pauni milioni 26 (kupanda hadi pauni milioni 33.5) kwake inaweza kuwa biashara kubwa, haswa ikiwa watapata mafanikio mengi katika miaka ijayo.

### #3. KALIDOU KOULIBALY KWENDA CHELSEA- PAUNI MILIONI 33

Hatimaye Kalidou Koulibaly ameondoka Napoli na kujiunga na klabu ya Ligi Kuu England baada ya kuhusishwa na kuhamia nchini humo kwa muda mrefu zaidi.

Mtu mwenye uzoefu wa hali ya juu na kipaji, Koulibaly alisaini Chelsea msimu huu wa majira ya joto kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 33. 'The Blues' walikuwa wanafahamu kuwa beki huyo wa kati alikuwa amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake kule Napoli na walipata fursa ya kumleta Stamford Bridge.

Hata hivyo, ujio wake unahisi kuwa muhimu kwa klabu hiyo ya Magharibi mwa London, ambayo imewapoteza Antonio Rudiger na Andreas Christensen msimu huu wa majira ya joto. Akiwa sehemu muhimu sana ya kikosi cha Napoli kwa miaka nane iliyopita, nyota huyo wa Kiafrika ana uwezo bora kwenye safu ya ulinzi. Zaidi ya hayo, pasi zake za masafa marefu, uwezo wa angani na sifa za uongozi zitakuwa muhimu sana katika kikosi cha vijana na chenye nguvu.

Thomas Tuchel anahitaji wachezaji ambao wanaweza kuwa sehemu ya kikosi cha kwanza chenye msimamo thabiti na pamoja na Thiago Silva, Koulibaly wanaweza kuunda ushirikiano wa ajabu wa beki wa kati msimu ujao.

Ingawa mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alifikisha umri wa miaka 31 Juni mwaka huu, umri ni namba tu kwake. Nidhamu yake, viwango vya utimamu wa mwili, na taaluma huweka njaa yake ya mafanikio, kwa hisani ambayo ada yake ya pauni milioni 33 inaonekana kama wizi kwa The Blues.

### #2. OLEKSANDR ZINCHENKO KWENDA ARSENAL- PAUNI MILIONI 30

Manchester City iliamua kuwaacha nyota wake kadhaa wa kikosi cha kwanza kuondoka msimu huu, baada ya kuwasili kwa Erling Haaland, Julian Alvarez, na Kalvin Phillips. Wakati Raheem Sterling akihamia Chelsea, Gabriel Jesus, na Oleksandr Zinchenko walisajiliwa Arsenal.

Ingawa Jesus aliondoka kwa pauni milioni 45, City ilimwachia Zinchenko kwa pauni milioni 30 tu (iliyopanda hadi pauni milioni 32). Ingawa mmoja amethibitisha uwezo wake zaidi ya mwingine, raia huyo wa Ukraine hajapata nafasi sawa kwani mara nyingi alitumiwa kama beki na kocha Pep Guardiola.

Lakini kocha msaidizi wa zamani wa Hispania, Mikel Arteta, hakika aliona umuhimu wa kumleta Zinchenko pale Emirates. Mchezaji anayeweza kubadilika sana, nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, anaweza kuchukua nafasi ya beki wa kushoto na nafasi ya kiungo.

Mchezaji bora wa mpira wa krosi na mkimbiaji bora zaidi, Zinchenko hutoa ulinzi mzuri katika nafasi ya beki wa pembeni huku pia akitoa usawa unaohitajika kwenye safu ya kiungo.

Kwa hiyo, kulipa pauni milioni 30 kwa mchezaji wa ubora na wasifu wa umri wa Zinchenko ni ajabu kwa timu ambayo haikufanikiwa kumaliza katika nne bora msimu uliopita.

### #1. KARIM ADEYEMI KWENDA BORUSSIA DORTMUND- PAUNI MILIONI 32.5

Sajili iliyopunguzwa kwa kila tafsiri ya maneno, Borussia Dortmund bado wamemnasa mchezaji bora zaidi, Karim Adeyemi.

Klabu hiyo ya Ujerumani ina ustadi wa kusajili mastaa wajao na kuwauza kwa faida kubwa baadaye. Kuondoka kwa Erling Haaland msimu huu wa majira ya joto ilikuwa ushahidi tosha, wakati kuwasili kwa Adeyemi kama mrithi kunaonyesha mkakati wao mzuri wa uhamisho.

Mshambuliaji huyo wa kati wa Ujerumani, ambaye alitimiza miaka 20 mwaka huu, alifunga mabao 33 na kutoa pasi za mabao 21 katika mechi 91 alizoichezea RB Salzburg kabla ya kuja Signal Iduna Park majira ya joto. Hii ni pamoja na mabao yake manne na asisti mbili katika mechi 11 za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa hiyo, Adeyemi tayari ana uzoefu mzuri wa kucheza katika kiwango cha juu na ataendeleza tu maendeleo yake katika klabu kama Dortmund. Pamoja na Giovanni Reyena, Jude Bellingham, Nico Schlotterback, na Donyell Malen, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani anaweza kuwa jambo kubwa linalofuata.

Ukuta wa 'njano' mara chache hukosa alama wakati wa kusaini vipaji vinavyokua, na kwa pauni milioni 35, Adeyemi anaweza kupata ada kubwa ikiwa ni wakati wataamua kumuuza. Lakini kwa sasa, straika huyo hakika ni usajili wa thamani ya fedha na atatoa matokeo mazuri wakati akijiandaa kufunga mabao kwao.

## Nukuu

"Ukweli ni kwamba mkataba wangu na Vipers ulikuwa wa miaka miwili, nimebakiza miezi miwili na Oktoba utamalizika, malengo yangu ni kucheza Simba, hivyo meneja wangu na Simba wako katika mazungumzo mazuri, kuhusu kutokucheza mechi dhidi ya Yanga ni kutokana na kutojisikia vizuri." **César Lobi Manzoki**



"Utakuwa ushirikiano mzuri kati ya Lukaku na [Lautaro] Martinez, wanaweza kuwa na upatina mzuri zaidi. Hisia nyingi, malengo mengi," **Ronaldo de Lima akipongeza kitendo cha Inter Milan kumsajili Romelu Lukaku.**



"Manchester United wanatakiwa kumruhusu [Cristiano] Ronaldo aondoke, si kwa sababu Ronaldo hawezi kucheza kwenye timu ya Ten Hag, hapana anaweza kucheza timu yoyote bali United bado hawajawa tayari kupigania kombe lolote kwa sasa," **Wayne Rooney**



# FUNIKA BOVU YA MIAKA 13 SIMBA DAY YA 14 LEO




Kiungo wa Simba, Jonas Mkude, ambaye ameshiriki matamasha yote 13 ya klabu hiyo, akiwa amevalia uzi mpya wa msimu huu. **PICHA: SIMBA**

**Na Adam Fungamwango**

MAADHIMISHO ya Tamasha la 14 la Simba Day yanatarajiwa kufanyika leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, timu hiyo itapocheza dhidi ya Saint George SC ya Ethiopia.

Ni mwaka wa 14 mfululizo kwa Simba kufanya tamasha hilo ambalo hulitumia kutambulisha wachezaji wake wa zamani, wapya iliyowasajili kwa msimu husika, jezi mpya huku likihanikizwa na mambo mbalimbali kama vile burudani kutoka kwa wasanii mbalimbali, ambapo huwa ni shughuli ya siku nzima. Klabu hiyo imetangaza kaulimbiu ya mwaka huu ambayo inaitwa 'We Are Unstoppable', ikiwa na maana ya 'Hatushikiki, Hatuzuiliki'. Kabla ya kilele cha leo, wanachama na mashabiki wa klabu hiyo walifanya shughuli za kijamii kama ilivyo kawaida yao miaka yote tangu lilipoanzishwa mwaka 2009, ambapo hutembelea sehemu mbalimbali hospitalini, shuleni, sokoni, makazi ya watoto yatima na watu wenye mahitaji maalum kwa ajili ya kutoa misaada.

**Hii itakuwa ni mechi ya 14 ya Simba kwenye tamasha lake. Katika mechi 13 ambazo imecheza imeshinda saba, sare mbili na kufungwa nne.**

Haya ni matokeo ya mechi zote 10 za Simba kwenye tamasha hilo...

**#1. Simba 1-0 SC Villa (2009)**

Mechi ya kwanza kabisa ya tamasha la Simba Day ilichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam dhidi ya SC Villa kutoka Uganda. Katika mechi hiyo, Simba ilishinda bao 1-0 likifungwa dakika ya nane na kiungo Mkenya aliyekuwa ndiyo kwanza amesajiliwa, Hirally Echessa.

**#2. Simba 0-0 Express (2010)**

Ikiwa chini ya kocha Patrick Phiri, na wachezaji kama Ally Mustapha 'Barthez', Emmanuel Okwi, Joseph Owino, Mohamed Banka, Patrick Ochan, Rashid Gumbo, Amri Kiemba, Mussa Hassan Mgosi, Jerry Santo, Simba ilishindwa kupata ushindi mwaka wa pili wa Simba Day ilipolazimishwa sare dhidi ya Express ya nchini Uganda katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**#3. Simba 0-1 Victory (2011)**

Simba ilikiona cha moto kwenye mwaka wa tatu kwa msimu wake wa Simba Day, ilipofungwa kwa mara ya kwanza baada ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Victory FC nayo ikitoka nchini Uganda.

Na kwa mara ya kwanza na mpaka sasa haijawahi kutokea, mechi hiyo ya Simba Day ilichezwa nje ya Dar es Salaam, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha. Likuwa ni bao la mkwaju wa penalti likifungwa dakika ya 70 na Patrick Sembuya.

**#4. Simba 1-3 Nairobi City Stars (2012)**

Kwa mara ya kwanza Simba ikacheza mechi yake ya Simba Day kwenye Uwanja wa Taifa (kwa sasa Benjamin Mkapa) mwaka 2012 dhidi ya Nairobi City Stars kutoka nchini Kenya. Ukawa ni msimu wa nne wa Simba Day. Ikiwa ni mara yao ya kwanza kucheza Taifa, Simba ilikubali kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa wageni wao. Dancun Owiti, Bruno Okullu na Boniface Onyango walipeleka maangalizi, kila mmoja akifunga bao, huku la kufutia machozi likifungwa na Mzambia Felix Sunzu.

**#5. Simba 4-1 SC Villa (2013)**

Baada ya kupoteza miaka miwili mfululizo, Simba ilirudi kwa kishindo kwenye Simba Day ya mwaka 2013, ilipoisasambua SC Villa ya Uganda mabao 4-1 kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Yalikuwa ni mabao ya Betram Mombeki aliyefunga mawili, Jonas Mkude na William Lucian 'Gallas', yaliyotosha kabisa kuwaangamiza wageni.

**#6. Simba 0-3 Zesco (2014)**

Simba ilikiona cha mtemakuni Simba Day ya mwaka 2013, ilipochapwa mabao 3-0 dhidi ya Zesco kutoka Zambia na kusababisha kupoteza kibarua kwa aliyekuwa kocha wake mkuu, Zdravko Lugarusic.

Walioifanya sherehe ya Simba Day kugeuka msiba ni Jackson Mwanza, Mayban Mwamba na Clautos Chama ambaye kwa sasa yupo Simba.

**#7. Simba 1-0 SC Villa (2015)**

Mwaka 2015 Simba iliingia mwaka wa saba wa tamasha hilo kwa kucheza na SC Villa kutoka Uganda. Katika mechi hiyo Simba ilishinda bao 1-0 likiwafanya mashabiki wa timu hiyo kuondoka na furaha uwanjani baada ya kipigo cha mabao 3-0 mwaka uliopita, bao lilifungwa dakika moja tu kabla ya mechi kumalizika na Awadh Juma.

**#8. Simba 4-0 AFC Leopards (2016)**

Simba ilitoa kipigo kitakatifu mbele ya AFC Leopards ya Kenya mwaka 2016 kwenye mechi ya mwaka wa nane wa Simba Day. Mabao ya Simba yalifungwa na Ibrahim Ajibu ambaye alifunga mawili, Mrundi Laudit Mavugo akifunga na Shiza Kichuya aliyekuwa akiichezea kwa mara ya kwanza akitokea Mtibwa Sugar.

**#9. Simba 1-0 Rayon Sport (2017)**

Pasi nzuri ya Emmanuel Okwi, ilimkuta Mohamed Ibrahim kwenye nafasi nzuri dakika ya 15 na kuujaza wavuni, ikawa ni bao pekee kwenye mechi hiyo iliyofanya Simba kuondoka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Rayon Sport kutoka nchini Rwanda.

**#10. Simba 1-1 Asante Kotoko (2018)**

Ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Simba kuleta timu kutoka Afrika Magharibi kwenye tamasha lake hilo. Timu kongwe Afrika, Asante Kotoko ilishuka nchini na kuilazimisha sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Mkapa. Obed Owussu aliifungia Kotoko bao, kabla ya Okwi kusawazisha.

**#11. Simba 3-1 Power Dynamos (2019)**

Ilikuwa ni 'hat-trick' ya Meddie Kagere, huku bao la kusawazisha la Power Dynamos ya Zambia likifungwa na Jimmy Dzindai, kona ikipigwa na Rally Bwallya.

**#12. Simba 6-0 Vital'O (2020)**

Simba ilicheza dhidi ya Vital'O ya Burundi, na kushinda mabao 6-0 ya Bernard Morrison, John Bocco, Clatous Chama, Ibrahim Ajibu, Chris Mugalu na Charles Ilamfya.

**#13. Simba 0-1 TP Mazembe (2021)**

Bao la Jen Baleke, liliizamisha Simba kwenye Simba Day ya msimu uliopita dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo.

Hayo ndiyo matokeo ya matamasha 13 yaliyopita kabla ya hili la mwaka huu litakalofanyika Uwanja wa Benjamin Mkapa leo kwa Simba kuikaribisha Saint George SC ya Ethiopia.

**JE, WAJUA?**



USHINDI wa mabao 2-0 dhidi ya Crystal Palace wiki iliyopita unamfanya Mikel Arteta kushinda jumla ya mechi 50 kati ya 98 alizoiongoza klabu hiyo kwenye Ligi Kuu England hadi sasa, hivyo anakuwa kocha wa pili klabuni hapo kushinda mechi nyingi zaidi kwa haraka baada ya Arsene Wenger aliyefanya hivyo baada ya mechi 94.





# Waziri aziamsha taasisi ubunifu teknolojia ya kilimo

**Na Magdalena Jackson,** SJMC

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amezitaka taasisi mbalimbali za utafiti kubuni teknolojia zitakazowasaidia wananchi kwenye sekta ya kilimo na mifugo.

Aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane Kanda ya Kati viwanja vya Nzuguni, jijini hapa.

"Ningependa tafiti zinazofanyika ziende kwa wananchi ili kuwasaidia kutoka kwenye hali duni vinginevyo utaalamu utabaki kwa wasomi pasipo kusaidia watu," alisema.

Kadhalika, alisema ubunifu watakaofanya uendane na vipato vya wananchi wa maisha ya kawaida.

Hata hivyo, alisema utafiti mwingi unaofanyika unaishia kwenye makaratasi na hauwafikii walengwa.

Alisema lengo la serikali kuandaa maonesho hayo ni kuyajengea uwezo wakulima na wafugaji mbinu bora za kuendeleza shughuli zao za kila siku kwenye maeneo yao.

Naye Mratibu wa maonesho hayo, Aziza Mumba, alisema kanda ya hiyo inaundwa na mikoa miwili ya Singida na Dodoma na taasisi, mashirika na kampuni mbalimbali zimeshiriki.

Alisema matarajio ni kila atakayetembelea maonesho hayo kwenda kutekeleza kwa vitendo anayojifunza katika eneo lake na kuwafundisha wengine ambao hawakupata fursa ya kuhudhuria kwenye maonesho.

Hata hivyo, alisema kutokana na uwapo wa tatizo la umiliki wa uwanja huo uendelezaji umesuasua kwa kipindi kirefu na mchakato wa kurejesha umiliki wa uwanja kwenye mikono ya serikali umekamilika baada ya kushinda kesi iliyokuwa inaendelea.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Sinyamule, alisema kazi kubwa iliyoko kwenye mkoa huo ni kuongeza tija katika ufugaji wa kisasa kutoka wa kienyeji pamoja na kuhamasisha kilimo cha umwagiliaji ili kupunguza kutegemea kilimo cha msimu wa mvua.

Senyamule alisema kuwa asilimia 79 ya wakazi wa mikoa ya Dodoma na Singida wanategemea kilimo, wanaendelea na kuwekeza nguvu kubwa katika kuwasaidia wananchi wa kanda hiyo ya kati.




Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri (wa tatu kushoto), akikata utepe kuzindua duka jipya la kisasa la Tigo, jijini mwishoni mwa wiki. Kulia kwake ni Kaimu Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Daniel Mainoya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 1/- kulipa madeni, askari wastaafu wa TRC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Reli nchini (TRC), limesema linaendelea kulipa madeni mbalimbali ikiwamo ya askari wastaafu 60 waliokuwa wakisafiri na treni za TRC wanaodai zaidi ya Shilingi bilioni moja.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo, Masanja Kadogosa, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akijibu maswali mbalimbali yaliyoulizwa na waandishi wa habari jijini hapo katika mkutano wa kueleza mwelekeo wa shirika hilo kwa mwaka 2022/23.

Kadogosa alisema mpaka sasa wamelipa Sh. bilioni 30 kwa wafanyakazi waliokuwa wakidai wakiwamo askari na wanaendelea kulipa madeni hayo baada ya kuhakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango na kwamba yapo madeni ya wastaafu wanaolidai shirika hilo tangu mwaka 2010.

Juzi gazeti hili lilichapisha habari kuhusu askari wastaafu kumwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuwasaidia kulipwa posho zao za kujikimu wanazoidai TRC. Akizungumza katika ofisi za IPP Dodoma, Sajenti mstaafu Severine Ngumba, alisema mpaka sasa wamefanya kila jitihada kufuatilia malipo yao bila mafanikio kwa zaidi ya miaka 10.

Ngumba, alisema kutokana na hali hiyo maisha yao na familia zao yamekuwa ya shida kwa kushindwa kumudu gharama za maisha ikiwamo ada kwa ajili ya watoto wao walioko shule.

Alisema fedha anazodai ni posho za kujikimu ambazo walizifanyia kazi walipokuwa watumishi katika kikosi hicho na walikuwa wakisindikiza treni za mizigo kwenda katika mikoa mbalimbali nchini.

"Mimi nimefanya kazi katika kikosi cha reli kwa miaka 21 na kazi ambazo tulikuwa tunazifanya ni kusindikiza treni ya mizigo ili kulinda watu na mali zao, kutoka Dar es Saalam kwenda Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Sinyanga, Mwanza, Kigoma hadi Mpanda, lakini tulikuwa hatulipwi na kama ukihoji tulikuwa tunawekwa mahabusu kwa madai kuwa tumegomea amri ya jeshi," alisema Ngumba.

Kadhalika, alisema wamejaribu kudai malipo hayo ya posho za kujikimu, lakini kila wanapopita hakuna walichofanikiwa zaidi ya kupigwa danadana.

"Tumehangaika vya kutosha bila majibu hadi leo hii kuja hapa kwa waandishi wa habari ili kutoa kilio chetu kwa viongozi wakuu wa nchi kuwaomba kusikia kilio chetu hiki cha muda mrefu kwani siyo sisi wapo askari wengi nchini na wengine wamekufa bila kupata haki zao," alisema.

Meja mstaafu wa jeshi hilo, Enock Mpilimi, alisema amefanya kazi katika kikosi hicho kwa miaka 34 na kwa mara ya mwisho kulipwa fedha hizo ni mwaka 2013. Alisema wakiwa kazini kabla ya kustaafu walikuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu kutokana na kusindikiza treni za mizigo bila malipo ya posho za kujikimu.

# Maofisa ugani watakiwa kuwafikia wakulima shambani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAOFISA ugani wameshauriwa kuwafikia wakulima mashambani ili kuwapatia huduma stahiki za kitaalamu ili kilimo chao kiwe na tija.

Mwezeshaji wa wakulima wa mikoa ya Morogoro, Dodoma na Singida, Peter Paula, kutoka kampuni ya Hans Agriculture Mashinery Limited, aliyasema hayo alipokuwa akitoa elimu kwa wakulima wa Wilaya ya Kondoa katika Maonesho ya Wakulima ya Nanenane jijini hapa.

Alisema wakulima wanahitaji kupatiwa huduma za kitaalamu ili kilimo kiwe na tija.

"Badala ya kufuatwa maofisini, watumie nafasi zao za kitaaluma za kilimo kwa kuwafuata wakulima hao huko mashambani ili wakatoe elimu jinsi ya kufanikisha kupata mazao yenye tija na ubora ili kuondokana na kilimo cha mazoea," alisema.

Paula ambaye kampuni yake inajihusisha na kutoa elimu ya mashine za kupanda mbegu na usambazaji kwa wakulima vijijini, alisema wakulima wengi hujikuta wanalima kwa mazoea kutokana na maofisa hao kutowafikia kwa wakati.

Naye mkulima wa mtama, Stella Chibita, alisema wakulima wanashindwa kubadilika katika kilimo chao kutokana na kutopatiwa utaalamu kwa wakati kutoka kwa maofisa hao.

Alisema kutokana na hali hiyo bado wakulima wataendelea kulima kilimo cha mazoea na watashindwa kupata mazao yenye tija yatakayowapa fursa ya masoko ndani na nje ya nchi.

Aliwataka wakulima kupitia maonesha hayo kutumia fursa ya kujifunza ili kuboresha kilimo chao.

Aidha, alisema kupitia maonesho hayo yatawasaidia wakulima kijiepusha na ununuzi wa mbegu zilizopitwa na wakati na vifaa vya kilimo feki.





## Serikali kuwezesha maofisa ugani ununuzi pembejeo

**Na Ashton Balaigwa,** MBEYA

SERIKALI imesema itatoa fedha kwa ofisa ugani wa kila kijiji nchini kwa ajili ya kununua pembejeo na mbegu za kisasa ili kulima shamba la ekari moja la zao linaloendana na ikolojia iliyoko eneo hilo ambalo pia litakuwa kama shamba darasa kwa ajili ya kujifunzia wakulima.

Pia serikali itatoa pikipiki kwa maofisa ugani hao ambazo zitafungwa mfumo wa mawasiliano ya GPS utakaomfanya kuonekana akifanya kazi hiyo ndani ya eneo lake na endapo ataitumia pikipiki hiyo tofauti na malengo yaliyokusudiwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo wakati alipotembelea banda la Wizara ya Kilimo ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), lililoko katika maonesho ya wakulima na wafugaji yanayofanyika kitaifa katika Viwanja vya John Mwakangale mkoani Mbeya.

Waziri Bashe alisema lengo la kutoa fedha hizo kwa kila ofisa ugani katika kijiji ni kutaka kuwabadilisha wakulima kulima kilimo cha kisasa na chenye tija kwa kutumia mbegu bora za teknolojia ya kisasa kwa kufuata ushauri wa kitaalamu.

"Kama ofisa ugani yupo katika ikolojia inayokubali kilimo cha alizeti, serikali itampatia fedha kwa ajili ya kununua mbegu na pembejeo zote ikiwamo mbolea ili aweze kulima katika shamba lake la ekari moja ambalo hilo hilo litakuwa shamba darasa la wakulima kujifunzia," alisema Waziri Bashe.

Alisema pia serikali itamtambua mkulima bora katika kila kijiji na kumpa fedha kwa ajili ya kununua mbegu na pembejeo kama ilivyo kwa ofisa ugani ili naye alime shamba la ekari moja kilimo cha kisasa nalo litumike kama shamba darasa.

Akizungumzia kuhusu pikipiki, alisema lengo lake ni kuwapatia usafiri maofisa ugani hao waweze kutoa huduma za kiugani katika maeneo yao ili kuongeza uzalishaji pamoja na tija hasa katika maeneo ya vijijini.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema mkakati wao ni kuongeza nguvu zaidi kwa kuwapatia mafunzo maofisa ugani ili waendelee kutoa elimu kwa wakulima.

Alisema mpango huo wa TARI unakusudia kuhakikisha kuwa wakulima wanapata mbinu bora za kilimo pamoja na teknolojia mbalimbali za kilimo ili kuongeza uzalishaji hasa kwenye mazao ya kimkakati.

# Zaidi bil. 300/- kuboresha miundombinu kiutalii

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imechukua mkopo wa zaidi ya Sh. bilioni 350 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya ndege, barabara huduma nyingine muhimu ili kumwezesha mtalii kufika kwenye vivutio vilivyoko kwenye Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini ikiwamo Ruaha, Kitulo na Katavi.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, alipozungumza na wanahabari kuhusu mikakati ya kutangaza na kuboresha vivutio mbalimbali vinavyopatikana Ukanda wa Kusini.

Alisema kwa kutambua umuhimu wa vivutio hivyo ambavyo vinachangia kwa kiasi kikubwa Pato la Taifa, serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imechukua mkopo kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya ndege katika kila Hifadhi ya Taifa ili kusaidia watalii kutua muda wowote na kila maeneo muhimu ambayo yatawekwa.

Alisema fedha hizo pia zitatumika kujenga na kuboresha njia zote zinazoingia na kutoka kwenye hifadhi ili kuwasaidia watalii kufika maeneo yote yenye historia mbalimbali za wanyama na uoto wa asili.

Tunaishukuru serikali kwa kukopa kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 350 ili kuwekeza kwenye hifadhi zote zinazopatikana Kusini naamini hatua hiyo itasaidia kuongeza na kuvutia watalii wengi zaidi kutoka ndani na nje ya nchi, tumezoea kuona idadi kubwa ya watalii Ukanda wa Kaskazini ni kutokana na uboreshaji wa miundombinu mbalimbali ikiwamo viwanja vya ndege, barabara na huduma nyingine muhimu za kijamii sasa ni zamu ya ukanda wa kusini alisema Prof. Sedoyeka.

Alisema serikali imejitahidi kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege katika hifadhi za Ukanda wa Kaskazini na kuna zaidi ya viwanja 40 barabara zinazofikika kwa urahisi ikilinganishwa na Ukanda wa Kusini, akitolea mfano Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kuwa na viwanja vya ndege visivyopungua sita.

"Kikubwa tunachokifanya kwa sasa ni kuhakikisha tunaboresha miundombinu katika hifadhi zote za Kusini na mradi huo utakamilika hadi mwaka 2025 na kazi nyingine ni kuweka mikakati ya namna ya kuvutia watalii ili mgeni anapofika katika hifadhi hizo apate huduma zote muhimu ikiwamo chakula na malazi," alieleza Prof. Sedoyeka.

Aidha, aliwaomba wadau wengine kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha mazingira kwa ajili ya kuvutia watalii kwa kujenga sehemu za kutoa huduma za malazi na chakula.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi, Mkuu wa Kanda ya Kusini, Steria Ndaga, alisema wanaendelea na jitihada za kuvitangaza vivutio vyote vinavyopatikana katika Hifadhi za Taifa zilizoko Kusini.

Alisema lengo la kutangaza vivutio hivyo ni kufungua fursa mbalimbali za uwekezaji ambazo zitawavutia watalii kutembelea hifadhi hizo na kutafuta taarifa sahihi za uhifadhi katika maeneo hayo.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashidi Chuachua, akimkabidhi funguo mshindi wa Bajaj wa promosheni ya Vodacom M-Pesa Imeitika mkazi wa Uyole jijini Mbeya, Georgina Misheli, katika hafla ya wiki ya tatu ya promosheni hiyo iliyofanyika viwanja vya Nanenane jijini humo. Wengine kushoto ni Magreth Mambai, Meneja Mkakati wa Masoko na Biashara na Ezekiel Nungwi, Mkuu wa Mauzo Vodacom Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TMA yatoa fursa wanaotaka huduma utabiri

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imewataka wadau wanaotaka kutoa huduma ya utabiri wa hali ya hewa kujisajili ili taarifa wanazotoa ziweze kuthibitishwa na mamlaka hiyo kwani ndiyo yenye jukumu na mamlaka kisheria.

Kauli hiyo ilitolewa jana na meneja huduma za hali ya hewa na kilimo nchini, Isack Yona, alipozungumza na Nipashe hatua zinazopaswa kuzingatiwa kwa wananchi wanaotaka kutoa huduma za hali ya hewa.

Alisema TMA iko tayari kutoa maelezo kwa wananchi, utaratibu unaotakiwa hadi kufikia kutoa taarifa za hali ya hewa na kuwa serikali imetoa fursa kwa wote watu waweze kushughulika kutoa huduma wajisajili na vituo vya pia ili kufanya shughuli hiyo.

Aliongeza kuwa endapo wakisajiliwa na mamlaka hiyo wahakikishe taarifa zinakidhi viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuhakikisha vinadhibitiwa na kukaguliwa.

"TMA iko tayari kutoa ufafanuzi kwa wananchi wanaotaka kufahamu taarifa mbalimbali za mamlaka hiyo kwa ajili ya kuwasaidia katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ikiwamo kilimo, jambo la muhimu ni kwa wale wanaotamani kufanya shughuli zetu kuhakikisha wanakuwa na taarifa sahihi kuhusu mamlaka, kujisajili na kufuata kanuni na sheria," alisema Yona.

Alidai kuwa TMA iko tayari kutoa ufafanuzi unaohitajika kwa wananchi kuhusu zoezi la utabiri wa hali ya hewa husasani kwenye shughuli za kilimo.

"Wadudu wengi kwenye mifugo na mimea chanzo chake ni hali ya hewa hata mabadiliko ya mwili wa binadamu pia yanasababishwa na suala hiyo, jambo la muhimu ni kwamba taarifa za hali ya hewa ni muhimu sana kwa ustawi na maendeleo ya taifa kwani zinatoa dira na muelekeo wa mambo yanayopaswa kufanywa," alisema Yona.

Akizungumzia kuhusu utabiri wa msimu mpya kwa kilimo nchini, Yona alisema kwa sasa hawawezi kutoa taarifa zozote mpaka mwezi oktoba mvua za vuli zitakapoanza kunyesha.

Aliwaomba wadau mbalimbali nchini kuwekeza kwenye vifaa vya utabiri wa hali ya hewa ili kusaidia upatikanaji wa taarifa maeneo mbalimbali kulingana na mahitaji. Joseph Ambindwile, mkazi kutoka Kata ya Ntaba wilayani Rungwe ambaye alifika katika banda la maonyesho la TMA, viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya yanapofanyika maonesho ya wakulima Nanenane alisema taarifa alizozipata kuhusu kilimo zimemsaidia kufahamu mambo anayopaswa kufanya kuelekea msimu mpya wa kilimo.

Aliiomba mamlaka hiyo kutoa taarifa mapema za kilimo ili wakulima wengine wajipange kuelekea msimu ujao kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu hao.






Gari lililobeba kreti za chupa za bia likiwa limepata ajali katika barabara ya mtaa wa Kariakoo Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mhadhiri aona haja kuwapo sheria ya kiislamu Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MHADHIRI kutoka Chuo Kikuu Zanzibar (ZU), Dk. Sikujua Omar Hamdani, amesema kuna haja ya kuwapo sheria ya kiislamu inayohusiana na haki ya ndoa, talaka na malezi ya watoto.

Alisema hayo jana wakati akiwasilisha maoni ya kuanzishwa sheria hiyo katika mkutano uliondaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) uliohudhuriwa na viongozi wa dini, wasaidizi wa sheria, wanasheria na wanaharakati wa kupinga udhalilishaji, uliofanyika Tunguu Ofisi za TAMWA.

Alisema imefika wakati Zanzibar kuwapo na sheria kama hiyo kwa sababu zilizoko hazikidhi matakwa ya utoaji haki kwa makundi hayo.

Aidha, alisema hatua hiyo itasaidia kuwapunguzia mzigo wa utoaji wa uamuzi makadhi wanaosimamia masuala ya kiislamu hasa katika masuala ya ndoa, talaka na malezi ya watoto.

Alisema zipo baadhi ya nchi kama Iraq, Malaysia, Sudan, Pakistan na Iran zinatumia sheria hiyo ambayo inatoa mwongozo kwa mahakimu na majaji wanaoendesha kesi katika mahakama za kadhi.

Alisema sheria hiyo licha ya kuwa itatumika maalumu kwa ajili ya Waislamu, lakini inaweza kuwa vifungu ambavyo vitatumika kwa ajili ya wasiokuwa waumini wa dini hiyo.

Naye Meneja miradi kutoka TAMWA, Ali Mohammed Abdalla, alisema taasisi hiyo miongoni mwa kazi zake ni kutetea haki za wanawake na watoto na uwapo wa sheria hiyo utaongeza matunzo kwa familia.

Msaidizi wa sheria kutoka Wilaya ya Magharibi 'A' Unguja, Fatma Khamis Ali, alisema sheria hiyo itaondoa changamoto na kasoro zilizoko katika sheria mbalimbali.

Kwa upande wake Mwanasheria Khamis Juma alisema, ujio wa sheria hiyo ni jambo zuri na itatoa mwongozo kwa makadhi wanapoamua masuala hayo ya kiislamu.

# Filamu 'Royal Tour' yaimarisha sekta utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdallah Juma Sadala (Mabodi), amesema filamu ya Royal Tour imesaidia kuimarisha sekta ya utalii Zanzibar.

Aliyasema hayo, juzi akifungua matembezi yaliyoandaliwa na Umoja wa Vijana Tanzania upande wa Zanzibar yenye lengo la kuhamasisha utalii wa ndani, sensa pamoja na kutangaza Ilani ya CCM ya mwaka 2022-2025, yaliyowashirikisha vijana kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema Rais Samia na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wapo mstari wa mbele kuhamasisha utalii na matokeo yanaonekana.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mjini Kichama, Talib Ali Talib, alisema wataendelea kusimamia utekelezaji ilani ya CCM na kuzipongeza serikali kwa hatua inazochukua kuimarisha utalii.

Naibu Katibu Mkuu wa UVCCM Taifa Zanzibar, Mussa Haji Mussa, alisema wataendelea kuunga mkono viongozi wao ili kuhakikisha taifa lina maendeleo.

Katibu wa hamasa na chipukizi UVCCM Taifa, Victoria Charles Mwanziva, alisema wamekuja kuunga mkono Royal Tour na kuangalia vivutio vya utalii vilivyoko Zanzibar.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa Wazazi, Othmani Ali Maulid, alisema ingawa shughuli hiyo iliandaliwa na vijana, jumuiya hiyo pia inaunga mkono jitihada zinzazofanywa na viongozi kuletea maendeleo taifa.

Matembezi hayo yalianzia Kisonge Mjini Unguja, maeneo ya historia ikiwamo visiwa vidogo hadi Kizimkazi mahali Rais Samia alikozaliwa.

# Wanawake watakiwa kuwajengea uwezo wenzao

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaib Ado, ameitaka ngome ya wanawake ya chama hicho kuwajengea uwezo wanawake wenzao ili wapate hamu ya kugombeaa nafasi za uongozi na kushiriki kwenye vyombo vya kutunga sheria katika chaguzi zinazokuja.

Aliyasema hayo jana Baitul Yamiin Milindi mjini Zanzibar akiwa katika sherehe za wanawake wa chama hicho zilizoandaliwa na ngome ya wanawake wa ACT-Wazalendo.

Alitaka wanawake wajengwe kimapambano ili wajiamini na baadaye wapate wagombea wazuri kutoka katika jamii ambao watakuwa viongozi baadaye.

"Ngome ya wanawake ya chama chetu ina wajibu wa kuwajenga uwezo wanawake ili kuwatoa hofu kushiriki katika uchaguzi na kupata wabunge, wawakilishi na madiwani kutoka miongoni mwao," alisema.

Alisema wanawake ndiyo wanaoleta ushindi katika chama chao na kwamba ni vyema kuimarisha ngome yao ili kutia hamasa katika kutafuta mabadiliko.

Alisema wako wanawake wengi wenye uwezo na sifa, lakini hawajui pa kuanzia na kuwa ngome hiyo itawaelimisha na watashiriki katika siasa na hatimaye kuingia katika chaguzi za kitaifa.

Aliwatoa hofu kwa kile alichokieleza kuwa siasa za nchi ni nzuri na zinaonyesha mwelekeo bora katika uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alitoa maagizo matano kwa ngome hiyo ikiwamo kuisimamia ajenda ya Tume Huru ya Uchaguzi kuelekea Katiba Mpya.

"Ngome ya wanawake iandae mpango wa kuongeza msukumo kwa kuandaa makongamano usiku na mchana ili kupata Tume Huru ya Uchaguzi na kuelekea Katiba Mpya," alisisitiza.

Katibu wa kikosi kazi cha ngome ya wanawake ACT-Wazalendo, Bonifasia Mapunda, alisema wanawake ni kundi lenye nguvu kubwa katika jamii kwa kuwa limebeba dhima ya jamii iliyoizunguka.

Naye Mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais, mama Zainab Kombo Shaib, aliwashauri wajasiriamali kuchukua mikopo kwa kujishughulisha na za kazi ya kilimo ambako kuna fursa nyingi.

Mjumbe wa Kamati Kuu, Ismail Jussa Ladhu, aliwataka wanawake hao kuomba fedha za ahueni ya UVIKO-19 ili ziwasaidie katika shughuli za maendeleo akisisitiza zimelengwa kuyawezesha makundi yote bila kujali itikadi za kisiasa.

# Ziara ya Pelosi Taiwan imevutia umakini

**Na George Muntu**

LICHA ya onyo la kujirudia la China, Spika wa Baraza la Wawakilishi la Marekani, Nancy Pelosi na ujumbe wake wa bunge waliwasili katika kisiwa cha Taiwan kwa ndege ya kijeshi ya Marekani Jumanne jioni kufanya ziara.

Kwa sababu ya nafasi bora ya Pelosi katika mfumo wa kisiasa wa Marekani, ziara yake imevutia umakini wa ulimwengu. Wizara ya Mambo ya Nje ya China ilitoa tamko la kulaani ziara hiyo baada ya Pelosi kuwasili Taiwan, na vikosi vya jeshi la China vimeanzisha mazoezi ya kijeshi kuzunguka kisiwa cha Taiwan, ikiwa ni pamoja na mazoezi ya ufyatuaji wa risasi za masafa marefu Taiwan katika mlango wa bahari, na mazoezi ya urushaji wa kombora ya kawaida katika mashariki mwa kisiwa hicho. Jeshi la Wanamaji la Marekani limetuma meli nne za kivita, pamoja na shehena ya ndege, mashariki mwa Taiwan ili kuhakikisha usalama wa Nancy Pelosi. Hali ya usalama katika eneo hilo imekuwa ya wasiwasi.

Kuna makubaliano mapana ya kimataifa kwamba Taiwan sio nchi, lakini ni sehemu ya Jamhuri ya Watu wa China. Hadi leo, Taiwan inasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya China iliyoanzishwa mnamo 1911. Mnamo Desemba 1949, Vikosi vya Wanajeshi vya Jamhuri ya China wakiongozwa na Chiang Kai-shek's wa Kuomintang walishindwa katika vita vya wenyewe kwa wenyewe vya China, na kulazimisha serikali ya Jamhuri ya China kuhamia Taiwan. Hili liliruhusu Chama cha Kikomunisti cha China kutangaza kuanzishwa kwa taifa jipya la China, Jamhuri ya Watu wa China, mwaka wa 1949.

Hata baada ya kushindwa vita na kukimbilia kisiwani, Taiwan bado imeendelea kujitambulisha kuwa Jamhuri ya China. Lakini, nchi kadhaa ziliendelea kuitambua Taiwan kama China, huku zingine zikiitambua China Bara, Jamhuri ya Watu wa China, kama serikali halali ya China.

Katika miaka ya 1960, nchi nyingi zilianza kubadili utambuzi wao wa Jamhuri ya China hadi Jamhuri ya Watu wa China kutokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya ardhi na idadi ya watu wa China ilisimamiwa na Jamhuri ya Watu wa China.

Mnamo Oktoba 1971, kikao cha 26 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilipitisha Azimio Na. 2758 lililokataa wawakilishi wa Chiang Kai-shek's kwenye viti vya Umoja wa Mataifa na mashirika yake yote husika, na kurejesha viti vya Jamhuri ya Watu wa China katika Umoja wa Mataifa, kumtambua mwakilishi wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kama mwakilishi pekee wa kisheria wa China katika Umoja wa Mataifa, na Jamhuri ya Watu wa China kama mmoja wa wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Tangu wakati huo, uwakilishi wa China katika mfumo wa Umoja wa Mataifa umetatuliwa kikamilifu.

Tarehe 1 Januari 1979, Marekani iliitambua Jamhuri ya Watu wa China kama serikali pekee halali ya China na kuanzisha nayo uhusiano wa kidiplomasia. Siku hiyo hiyo, Marekani iliondoa utambuzi wake wa Jamhuri ya China na kusitisha uhusiano wa kidiplomasia nayo.

Ni muhimu pia kutambua kwamba mwaka 1972, 1978 na 1982, Marekani ilitia saini matamko rasmi matatu ya pamoja na China ambazo zote zinathibitisha kuwa kuna China moja tu duniani na Taiwan ni sehemu ya China, na kwamba Marekani itaondoa majeshi yake na mitambo ya kijeshi kutoka Taiwan. Tamko la pili na la tatu la pamoja lilienda mbali zaidi kwa kusema kwamba Marekani inaitambua Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuwa serikali pekee ya kisheria ya China, na kwamba watu wa Marekani watadumisha mahusiano ya kitamaduni, kibiashara na mengine yasiyo rasmi na watu wa nchi hiyo ya Taiwan.

Kwa kuwa Pelosi ni mwanasiasa wa nafasi ya tatu katika utaratibu wa kisiasa wa Marekani na Bunge la Marekani ni sehemu muhimu ya serikali ya Marekani, ziara ya Pelosi nchini Taiwan kwa vyovyote vile haiwezi kuwa sio rasmi, hivyo inapaswa kuzingatiwa kama ukiukaji wa ahadi ya Marekani katika matamko rasmi matatu yaliyotajwa hapo juu.

Kwa kuzingatia uzito mkubwa wa Pelosi katika siasa za Marekani, ziara yake nchini Taiwan itatafsiriwa bila shaka na majeshi ya uhuru wa Taiwan kwenye Kisiwa cha Taiwan kama msaada mkubwa wa kisiasa wa serikali ya Marekani kwa uhuru wa Taiwan.

Kwa miaka mingi, Marekani imevunja ahadi yake kwamba haiungi mkono uhuru wa Taiwan. Maofisa wake wakuu wa serikali na wabunge wamefanya ziara za mara kwa mara katika kisiwa hicho cha China. Zaidi ya hayo, inaendelea kuiuzia silaha Taiwan, na kuhimiza serikali ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo kutumia nguvu za kijeshi kuzuia muungano wa Taiwan na China bara.

Inapaswa kueleweka kuwa China, kama nchi huru, ina kila sababu ya kujilinda na kulinda maeneo yake kwa njia yoyote. Na kuitaka Marekani kuheshimu kanuni ya China moja.

***(Mwandishi ni mchambuzi wa masuala ya siasa za kimataifa na mambo ya nje aliyepo jijini Dar es Salaam. Barua pepe: cleophacegeorge@gmail.com)***



Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, akisalimiana na mmoja wa wazee anayehudumiwa katika Makazi ya Wazee Njoro Moshi mkoani Kilimanjaro katika ziara yake ya kukagua huduma zinazotolewa katika makazi hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwigulu ataka taasisi kuchagiza maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameitaka Taasisi za Maendeleo ya Fedha (DFIs), kushiriki kikamilifu kuchagiza maendeleo endelevu ya kiuchumi kupitia Mpango wa Viwango Endelevu na Uthibitishaji (SSCI).

Alisema mpango huo unatoa viwango vya jumla na thabiti ili kuzifanya taasisi za fedha zinazoendeshwa na thamani ziwe thabiti na zenye faida.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano rasmi wa DFIs kwa ukanda wa Afrika Mashariki kujadili Masuala ya Viwango Endelevu uliofanyika Dar es Salaam, alisema SSCI inalenga kuzisaidia taasisi hizo kuongeza ubunifu na kujiendeleza kidijitali na kuwa uendelevu ili kuongeza tija na ufanisi katika utunzaji wa mazingira na kuchagiza uchumi jumuishi na endelevu.

"Viwango vya SSCI ni muhimu kwa ajili ya kuzijengea uwezo DFIs zetu, ili kuzifanya taasisi zetu kuwa thabiti na zenye kuleta faida kwa muda mrefu," alisema.

Dk. Nchemba aliongeza kuwa SSCI inasaidia kuhakikisha mipango na mikakati ya taasisi zilizoidhinishwa zinaendana na SDGs na Mkataba wa Hali ya Hewa ya Paris, ili kuwiana na vipaumbele vya maendeleo ya taifa.

"Wito wangu kwenu ni kuwa tayari kujizatiti na kutekeleza masuala yote muhimu yanayokubaliwa na SSCI, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kufadhili maendeleo endelevu na kushughulikia changamoto za kimataifa zinazotukabili ikiwa ni pamoja na umaskini, mabadiliko ya tabia nchi, na uharibifu wa mazingira, " alisisitiza Dk. Nchemba.

Awali Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo (TIB), Lilian Mbassy, alisema mkutano huo ulilenga kujadili majukumu yanayoweza kufanywa na DFIs kupitia SSCI

# Fundi seremala ajinyonga madai kuzidiwa madeni

**Na Said Hamdani,** LINDI

FUNDI seremala mkazi wa Tandika, jijini Dar es Salaam, Omari Mpilu (59), anadaiwa kujinyonga kwa kutumia shuka kwa madai ya kuelemewa na madeni.

Kamanda wa Polisi mkoani Lindi, Marko Chilya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa alijinyonga kwenye nyumba ya kulala wageni Kata ya Somanga, Tarafa ya Miteja, wilayani Kilwa mkoani Lindi.

Alisema fundi huyo alifika kwenye nyumba hiyo na kuchukua chumba, lakini majira ya saa nne asubuhi, wahudumu waligonga chumba chake bila mafanikio na kuamua kuvunja mlango na kukuta amejinyonga.

Chilya alisema walipoingia walikuta amefunga shuka kwenye nondo ya dirisha na kujinyonga, ndipo walipotoa taarifa Kituo cha Polisi Somanga.

"Baada ya askari kufika eneo la tukio wameukuta mwili ukiwa unaning'inia dirishani huku simu yenye laini tatu na begi likiwa mezani," alisema.

Kamanda Chilya alisema baada ya upekuzi walikuta kamba mbili aina ya manila zenye urefu wa mita tano na sentimita 1.5, huku uchunguzi wa awali ukionyesha kuwa alizidiwa na madeni na kuamua kwenda Somanga kujificha.

Alitoa wito kwa wananchi wanapokuwa na shida za maisha kutochukua uamuzi mgumu wa kudhuru maisha yao na kushauri kuacha kujiingiza kwenye mikopo isiyo na tija.

HABARI KIMATAIFA

# Taiwan yaijibu China mazoezi ya kijeshi

**TAIPEI,** Taiwan



TAIWAN imesema imejibu mazoezi ya kijeshi ya Wachina ambayo sasa ni siku yao ya nne kwa kupeleka ndege na meli katika lango la bahari la kisiwa hicho.

Mvutano huo ulikuja baada ya ziara ya ujumbe wa Marekani ukiongozwa na kiongozi mkuu wa Chama cha Democrat, Nancy Pelosi, katika kisiwa cha Taiwan kinachojitawala, licha ya China kudai kuwa Taiwan ni sehemu ya nchi hiyo. Inaelezwa kuwa China inaiona ziara hiyo kama changamoto kwa madai yake ya kujitawala juu ya Taiwan, ambayo inajiona kuwa tofauti.

Wizara ya ulinzi ya Taiwan ilisema meli na ndege za China zilifanya mazoezi ya kutaka kushambulia katika mlango wa Bahari wa Taiwan mwishoni mwa wiki iliyopita, huku baadhi zikivuka mstari wa kati unaotenganisha pande hizo mbili.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, Jeshi la Taiwan lilijibu ipasavyo mazoezi makali ya moja kwa moja, ambayo ilielezea kama shambulio la kuigiza kwenye kisiwa hicho, kwa kutuma ndege na meli nyingi asubuhi ya jana.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Taipei, Waziri Mkuu wa Taiwan, Su Tseng-chang, aliishutumu China kwa kile alichokiita kiburi kutumia mazoezi hayo kuvuruga uthabiti wa kikanda, huku akiomba China ijizuie.

Aidha, Beijing haijazungumzia mazoezi ya hivi karibuni ya mfululizo wake wa siku nne wa mazoezi ya kijeshi angani na baharini karibu na Taiwan.

### CHINA YATUPIWA LAWAMA

Msemaji wa Ikulu ya White House, alisema shughuli hizo ni ongezeko kubwa la juhudi za China za kubadilisha hali ilivyo sasa.

"Ni za uchochezi, hazijibiki na zinaongeza hatari ya kufanya makosa, pia wanakinzana na lengo letu la muda mrefu la kudumisha amani na utulivu katika mlango wa Bahari wa Taiwan, jambo ambalo ulimwengu unatarajia," alisema.

China ilisema ziara ya Pelosi ilitishia sana amani na utulivu katika mlango wa Taiwan.

Inasema inaiona Taiwan kama jimbo lililojitenga ambalo hatimaye litakuwa chini ya udhibiti wa Beijing, mbali na kuwa Taiwan ni kisiwa kinachojitawala ambacho kinajiona kuwa tofauti na China.

Beijing pia ilitangaza kuwa inasitisha ushirikiano na Marekani katika maeneo kadhaa muhimu ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, mazungumzo ya kijeshi na jitihada za kupambana na uhalifu wa kimataifa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken aliishutumu China kwa kuchukua hatua zisizowajibika kwa kuzuia njia muhimu za mawasiliano na Washington.

Pelosi anayetajwa kuwa mkosoaji wa muda mrefu wa China na mwanasiasa wa ngazi ya juu zaidi wa Marekani kusafiri katika kisiwa hicho katika miaka 25, alitembelea Taiwan, licha ya Beijing kutoa onyo juu ya kiongozi huyo kukanyaga eneo hilo.

Akiwa Taiwan Pelosi, alisema kuwa ulimwengu unakabiliwa na chaguo kati ya uhuru na demokrasia na kwamba China haiwezi kuzuia viongozi wa dunia kuzuru kisiwa hicho.

"Inasikitisha kwamba Taiwan ilizuiwa kushiriki katika mikutano ya kimataifa, ambayo hivi karibuni zaidi ilikuwa Shirika la Afya Ulimwenguni, kutokana na pingamizi la Chama cha Kikomunisti cha China," alisema Pelosi.

Mamlaka ya China inakiona kisiwa hicho kinachojitawala kama sehemu ya eneo lake na inasisitiza kuwa inapaswa kuunganishwa na bara, kwa nguvu ikiwa ni lazima.

Inaelezwa kuwa kisiwa hicho kina katiba yake, viongozi waliochaguliwa kidemokrasia, na takriban wanajeshi 300,000 wanaofanya kazi katika vikosi vyake vya jeshi.

Vile vile inatajwa kuwa ni nchi chache tu zinazoitambua Taiwan, huku wengi wakiitambua serikali ya China iliyoko Beijing badala yake, ambapo Marekani haina uhusiano rasmi na Taiwan lakini ina sheria inayoitaka kukipa kisiwa hicho njia ya kujilinda. **BBC**

## Rais Zelensky asifu mafanikio ya jeshi la Ukraine

**KYIV,** Ukraine

RAIS wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, amelisifu jeshi la nchi yake kwa kuendesha operesheni kabambe za kujibu mapigo dhidi ya vikosi vya Russia.



Akizungumzia kupitia ujumbe wa video alioutoa usiku wa kuamkia jana, Zelensky alisema katika kipindi cha wiki moja iliyopita jeshi la Ukraine limepata mafanikio makubwa kwa kuharibu mikakati ya jeshi la Russia.

"Kila shambulizi kwenye maghala ya silaha ya adui, kwenye vituo vyao vya operesheni na dhidi ya vifaa vyao vya kijeshi linanusuru maisha ya sisi sote, wanajeshi wa Ukraine na raia," alisema Zelensky.

Aliongeza kuwa vikosi vya Ukraine vimemudu kuyakomboa baadhi ya maeneo lakini sehemu kubwa ya majimbo hayo bado yanadhibitiwa na Russia.

Kiongozi huyo pia alishukuru juu ya mchango wa msaada wa silaha kutoka mataifa washirika yakiwamo ya magharibi kwa kuipelekea silaha nchi yake. **DW**




Mwanasiasa Mkuu wa Marekani, Nancy Pelosi, akiondoka Taiwan Jumatano ya wiki iliyopita baada ya kumaliza ziara yake. **PICHA: BBC**

## Uganda yachukua hadhari kipindi cha mpito

**KAMPALA,** Uganda

MAMLAKA nchini Uganda zimewataka wafanyabiashara kujiweka sawa kukabiliana na wiki ngumu wakati Kenya ambayo ni njia kuu ya kusafirisha bidhaa inafanya uchaguzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, ilieleza kuwa hakuna ushahidi wa kuaminika wa tishio la usalama ambalo linaweza kuvuruga operesheni za usafirishaji katika njia ya kaskazini, huku wafanyabiashara wakishauriwa kuchukua tahadhari kwa kuchelewesha uagizaji bidhaa au kutumia njia mbadala ya kati.

Uganda pia iliwashauri raia wake wanaoishi na kufanya kazi nchini Kenya kuchukua tahadhari, baada ya Marekani kutoa ilani ya kusafiri kwa wale wanaotembelea mji wa Kisumu.

Ilisema suala hilo lilikuja baada ya Rais Uhuru Kenyatta na maofisa wake kuihakikishia kanda nzima kuwa uchaguzi unaotarajiwa kufanyika kesho nchini humo utakuwa wa amani na kwamba hata wagombea wa urais William Ruto na Raila Odinga pia waliahidi amani na kukubali kushindwa iwapo upigaji kura utakuwa huru na wa haki.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uganda Henry Okello, alisema anatarajia uchaguzi utamalizika kwa salama lakini wanajiandaa na hali yoyote itakayojitokeza ikiwa na mbinu mbadala ya kuwa na akiba ya bidhaa muhimu na kubadilisha njia ya usafirishaji bidhaa kupitia Tanzania. **VOA**

## HABARI MICHEZO

# NMB MARATHON 2022 YAZINDULIWA, KUKUSANYA MIL. 600/- KUTIBU FISTULA

**Na Mwandishi Wetu**

MSIMU wa pili wa Mbio za Hisani za NMB Marathon, zitakazofanyika Septemba 24, mwaka huu na kuhudhuriwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, umezinduliwa, lengo likiwa ni kukusanya kiasi cha Sh. milioni 600 kusaidia matibabu ya kinamama wanaosumbuliwa na maradhi ya fistula katika Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam.

**Uzinduzi wa NMB Marathon 2022, zinazoandaliwa na Benki ya NMB, ulifanyika Jumamosi iliyopita katika Viwanja vya Leaders vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam, ukienda sambamba na mbio za majaribio za kilomita 10 na 21, na michezo mingineyo, huku mgeni rasmi akiwa ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna.**

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, ulioshirikisha waalikwa kutoka kampuni, taasisi na vikundi mbalimbali vya mbio za taratibu (jogging), Zaipuna alisema baada ya mafanikio katika mwaka wa kwanza wa mbio hizo (2021), NMB inaamini malengo ya miaka minne yatakamilishwa katika mbio za mwaka huu.

“Mwaka jana tulizindua mbio hizi za hisani tukishirikiana na CCBRT, tukaziita NMB Marathon chini ya kaulimbiu isemayo ‘Mwendo wa Upendo’. Lengo likiwa kukusanya kiasi cha Sh. bilioni moja katika kipindi cha miaka minne, kwa maana ya Sh. milioni 250 kwa kila mwaka.

“Lakini tukapata mafanikio makubwa yaliyotuwezesha kukusanya Sh. milioni 400, ambazo tulizipeleka CCBRT na kusaidia kinamama mbalimbali waliokuwa na tatizo la fistula. Mwaka huu, tumeona haja ya kuweka lengo la kukusanya Sh. milioni 600 ili kutimiza Sh. bilioni moja ndani ya miaka miwili,” alisema Zaipuna.

Ofisa Mtendaji Mkuu huyo aliwashukuru wadhamini wakubwa wa NMB Marathon, Kampuni za Bima za Sanlam na UAP, pamoja na washiriki waliochangia kurejesha tabasamu kwa kinamama kwa kulipia gharama za matibabu yao, huku akiwataka Watanzania zaidi kujitokeza ili kupata Sh. milioni 600 zitakazosaidia kuendelea kuwasaidia kinamama wengi zaidi.

“Mbio hizi zitafanyika Septemba 24, mwaka huu, zitaanzia na kumalizikia hapa Leaders Club, ambako mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye tulikuwa naye katika mwaka wa kwanza wa mbio hizi, tayari ametuthibitishia kuwa tutamaliza naye mchakato huu wa kukusanya Sh. milioni 600,” alisema Zaipuna.

Naye Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi, aliishukuru NMB kwa wazo zuri lililozaa Mbio za NMB Marathon, ambazo zimesaidia kukusanya pesa kusaidia kinamama wanaohitaji msaada wa kitiba kumaliza tatizo la fistula, ambalo linawakabili takriban kinamama 3,000 kwa mwaka.

“Niwashukuru sana NMB kwa sababu sidhani kama kuna benki iliyowahi kutoa ahadi ya kusaidia Sh. bilioni moja ya matibabu ya fistula. Tatizo hili ni kubwa nchini, kwani ukiondoa kinamama 3,000 wanaopata tatizo hilo kila mwaka, wapo wagonjwa wa zamani wanaoendelea kusumbuliwa na tatizo hili.

“Kuna maeneo mawili yanayosababisha kinamama kuendelea kusumbuliwa na fistula, la kwanza likiwa ni elimu. Jamii haina elimu ya kutosha juu ya tatizo hili, kwamba bado tatizo hili halieleweki na jamii inawatenga wanawake wanaokumbwa na maradhi haya, yanayohusishwa na imani za kishirikina,” alisema.

Aliongeza kuwa tatizo la pili ni gharama kubwa, kuanzia za usafirishaji wa wagonjwa kutoka waliko hadi hospitalini kwake, gharama za matibabu, pamoja na malazi na chakula wakati wakiendelea na matibabu, hivyo NMB imeona mbali kusaidia kada hiyo muhimu katika jamii.

Alisema kupitia Sh. milioni 400 za NMB Marathon 2021, CCBRT iliweza kupambana na changamoto hizo mbili zinazokosesha tiba kwa akina mama wenye fistula, ambazo ziligharamia tiba ya wanawake 60, pia zilitumika kuzunguka katika mikoa minne ya Rukwa, Kagera, Mtwara na Songwe kutoa elimu.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (wa tatu kushoto), Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Hospitali ya CCBRT, Brenda Msangi (aliyevaa kofia), pamoja na maofisa wengine wa benki hiyo wakishiriki kwenye mbio katika viwanja vya Leaders Dar es Salaam kuashiria uzinduzi wa NMB Marathon 2022. NMB Marathon 2022 (Mwendo wa Upendo), ni maalum kwa ajili ya kuchangia wagonjwa wa fistula katika Hospitali ya CCBRT. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Coastal kamili kwa KMC, Yanga

**Na Cheji Bakari, Tanga**

IKIWA imebaki takriban wiki moja kabla ya pazia la Ligi Kuu Bara msimu wa 2022/23 kufunguliwa rasmi Agosti 15, mwaka huu, uongozi wa timu ya Coastal Union umesema kikosi hicho kimekamilika kwa ajili ya ligi hiyo.

Agosti 17, Coastal Union itashuka dimbani kucheza mechi yake ya kwanza msimu huu kwa kuvaana na KMC ya Dar es Salaam katika Uwanja wa Mkwakwani kabla ya Agosti 20, mwaka huu kuikaribisha Yanga katika mechi yake ya pili ya nyumbani katika dimba hilo.

Akizungumza na mwandishi wetu jijini Tanga jana, Msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi, alisema licha ya kikosi hicho kuondokewa na nyota wake muhimu ambao waliipa nguvu timu hiyo msimu uliopita, lakini bado kina wachezaji wazuri watakaoleta ushindani msimu huu.

“Kikosi kipo kambini, wachezaji wanaendelea kujifua na wote wapo vizuri, hata wale walioondoka nafasi zao zimezibwa, kuna wachezaji tuliwatoa kwa mkopo Dodoma Jiji, Ruvu Shooting na Mbeya Kwanza, wote wamerudi hivyo hatuna wasiwasi katika hilo.

## Wavu raundi ya kwanza tamati leo

**Na Hadija Mngwai**

MICHUANO ya mchezo wa Wavu Ligi ya Taifa raundi ya kwanza iliyokuwa ikiendelea kutimua vumbi kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamini Mkapa, inafikia tamati leo huku timu kadhaa zikitoshana nguvu juzi.

Katika michezo iliyochezwa juzi kwa upande wa wanawake, timu ya UDSM iliambulia kichapo cha seti 3-0 dhidi ya Kampala na Jeshi Stars iliibuka na ushindi wa seti 3-0 dhidi ya NHIF wakati Star Girls ilijikuta ikiibuka na ushindi wa seti 3-0 dhidi ya Golden Wings na Magereza yenyewe ikiibamiza Mafinga Parish kwa seti 3-0.

Kwa upande wa wanaume, Mipango iliibuka na ushindi wa seti 1-3 dhidi ya Kampala na Kigamboni ikipoteza kwa seti 3-0 dhidi ya Kigamboni wakati Tanesco yenyewe ikiibamiza Serengeti kwa seti 3-0.

# Manara amponza Hersi Siku ya Mwananchi Yanga

**Na Adam Fungamwangwo**

BAADA ya kuonekana juzi akitangaza kikosi cha wachezaji wa timu hiyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam huku akiwa kwenye kifungo, Sekretarieti ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), limewafunguliwa mashtaka ya kimaadili Rais wa Yanga, injinia Hersi Said na Mhamasishaji wa klabu hiyo aliyefungiwa, Haji Manara.

Taarifa iliyotokea jana na (TFF) ikisainiwa na Ofisa Habari na Mawasiliano wa shirikisho hilo, Cliford Ndimbo, imeeleza kuwa Kamati ya Maadili hivi karibuni ilimfungia miaka miwili Manara kujihusisha na shughuli yoyote ya mpira wa miguu, lakini ameshidwa kutekeleza adhabu hiyo.

Naye, Injinia Hersi, taarifa hiyo imeeleza kuwa amefunguliwa mashtaka kwa kwenda kinyume na ibara ya 16 (1) (a) ya Katiba ya TFF, pamoja na ibara ya 1 (6) ya Katiba ya Yanga.

Ilisema baada ya Manara kuadhibiwa na Kamati ya Maadili ya TFF, Sekretarieti ilimwandikia barua Hersi kuhakikisha klabu inaheshimu uamuzi huo.

Taarifa ilisema kuwa mwenyekiti wa kamati hiyo amepelekewa mashtaka hayo, walalamikiwa watapewa mashtaka na wito baada ya kamati kupanga tarehe ya kusikiliza mashtaka hayo.

Juzi katika hali isiyoshangaza wengi, Manara ambaye hivi karibuni alifungiwa kutojihusisha na soka kwa kipindi cha miaka miwili na faini ya Sh. milioni 20 na Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), aliingia uwanjani na kuanza kuwatambulisha wachezaji wa msimu ujao wa timu hiyo pamoja na benchi la ufundi.

Manara alifungiwa baada ya kupatikana na kosa la kumtolea maneno yasiyofaa Rais wa TFF, Wallace Karia kwenye mechi ya fainali ya Kombe la FA kati ya Yanga na Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Julai 2, mwaka huu.

Baada ya kumaliza kutambulisha wachezaji, Manara alisema aliingia hapo kama mshereheshaji mwingine yeyote kwenye shughuli za kijamii na si msemaji wa klabu hiyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SANE ATAKIWA UNITED



KLABU ya Manchester United imewasiliana na Bayern Munich kuhusu uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Manchester City, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

### LIVER NAYO KWA SANE

LIVERPOOL pia wana nia ya kuwasilisha ombi la kutaka kumsajili Leroy Sane ambaye ni winga wa Ujerumani. ***(Liverpool Echo)***

### CHELSEA WAKOMAA NA JONG

CHELSEA wametoa euro milioni 70 pamoja na beki wa kushoto wa Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 31, kwa lengo la kumnunua kiungo wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Sport)***

### DE BEEK, DE JONG KUPISHANA



KLABU ya Manchester United inaweza kumtoa kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 25 katika makubaliano ya kubadilishana na Frenkie De Jong. ***(Express)***

### RUZI KUNG'OLEWA NAPOLI

KLABU ya Manchester United pia inamtaka kiungo wa kati wa Napoli na Hispania, Fabian Ruiz mwenye umri wa miaka 26, kama mbadala wa Frenkie De Jong. ***(Goal)***

### BOURNEMOUTH KWA SENESI

KLABU ya Bournemouth ipo tayari kumsajili beki wa kati wa Feyenoord na Argentina, Marcos Senesi mwenye umri wa miaka 25. ***(Fabrizio Romano)***

### CHELSEA KUMKOSA SESKO



MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg kutoka Slovenia, Benjamin Sesko mwenye umri wa miaka 19, ameamua kubaki katika klabu hiyo ya Austria msimu huu licha ya Chelsea na Manchester United kumtaka. ***(Sky Sport Austria)***


### GAKPO NAYE MAWINDONI

KLABU ya Manchester United imemwongeza winga wa Uholanzi na mchezaji bora wa mwaka wa Uholanzi, Cody Gakpo, 23, kwenye orodha yao ya uhamisho kutoka PSV Eindhoven. ***(Mirror)***

### KIPA AMULIKWA UNITED

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag ana jukumu kubwa katika harakati za klabu hiyo kutafuta kipa wa pili nyuma ya David de Gea baada ya uhamisho wa mkopo wa Dean Henderson kwenda Nottingham Forest. ***(Sun)***

### CUCURELLA NA BRIGHTON



MMILIKI wa Chelsea, Todd Boehly alimsafirisha beki wa kushoto wa Hispania, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 24 hadi Mykonos nchini Ugiriki ili kukamilisha uhamisho wake kutoka Brighton. ***(Athletic)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP ALIA LIVERPOOL KUANZA VIBAYA EPL

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amekiri kwamba, timu yake ya Liverpool haikustahili pointi tatu wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 Jumamosi dhidi ya Fulham, akikosoa 'mtazamo' wa wachezaji wa 'Wekundu' hao namna walivyoanza msimu.

**Fulham inayonolewa na Marco Silva iliwakimbiza Liverpool katika kipindi cha kwanza, na kupata bao la kuongoza kupitia kwa Aleksandar Mitrovic kwenye mchezo huo wa kwanza wa Ligi Kuu England.**

Darwin Nunez aliingia akitokea benchi na kusawazisha katikati ya kipindi cha pili, kabla ya Mitrovic kufunga kwa mkwaju wa penalti baada ya kufanyiwa faulo na Virgil van Dijk.

●●● Hatukuwa kwenye kiwango bora na mtazamo wa wachezaji ulikuwa tofauti kabisa, tulifanya...

Mohamed Salah akaisawazishia Liverpool na kuwawezesha kuondoka na pointi moja kwenye mchezo huo.

Akizungumza na BT Sport baada ya mchezo, Klopp alifichua kwamba, alikasirishwa na mwanzo wa Liverpool na alielezea hisia zake wakati wa mapumziko.

"Jambo zuri zaidi kwenye mchezo ni matokeo, kwamba tunapata alama kutoka kwa mchezo mbaya kutoka kwa upande wangu," alisema.

"Mtazamo haukuwa sawa mwanzoni, tulitaka kupigana, lakini hatuoni kuwa ni rahisi zaidi.

"Matokeo ni mazuri, hatustahili zaidi ya hayo, lakini tutanakiwa kucheza zaidi ya hapa."

Aliongeza: "Huwezi kuwaacha vijana wacheze kwa mtazamo tofauti. Hatukuwa kwenye kiwango bora na mtazamo wa wachezaji ulikuwa tofauti kabisa, tulifanya tofauti kabisa na tulivyotakiwa.

"Kila mtu alikuwa chini ya shinikizo. Hatukuwa na kasi, tungeweza kushinda mchezo kwani tulikuwa na nafasi kubwa, lakini hatukuweza."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
WEST BROMWICH
VERSUS
WATFORD
1 | 2.35
X | 3.10
2 | 3.00

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI AANZA KUMKOSHA GALTIER




**PARIS,** Ufaransa

KOCHA Mkuu wa Paris Saint-Germain, Christophe Galtier, amemsifia Lionel Messi kwa kutatua changamoto za msimu uliopita na kuwa na mwanzo wa "msimu mzuri" baada ya kufungua msimu wa Ligi Kuu ya Ufaransa kwa mabao mawili.


Messi alihitimisha ushindi wa PSG wa 5-0 dhidi ya Clermont Jumamosi kwa mabao mawili ya dakika za lala salama, likiwamo bao la kuvutia la kichwa. Neymar, Achraf Hakimi na Marquinhos wote walifunga katika kipindi cha kwanza.

Mabao mawili ya Muargentina huyo yanakuja baada ya kufunga mabao 11 pekee katika michuano yote kwenye msimu wake wa kwanza katika mji mkuu huo wa Ufaransa baada ya kuhama kutoka Barcelona, huku akihangaika kupata mshikamano pamoja na Neymar na Kylian Mbappe msimu uliopita.

"Alikuwa na msimu mgumu kidogo msimu uliopita," alisema Galtier akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Kulikuwa na mabadiliko makubwa, lakini katika kila msimu kabla ya hapo ana angalau mabao 30. Na sasa ameanza na msimu mpya vizuri sana."

Galtier, ambaye alichukua mikoba ya PSG kutoka kwa Mauricio Pochettino mwezi uliopita, alimsifu Messi baada ya kuzungumza kwa kirefu wakati Messi wa ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Japan.



## 'Alonso anakwenda Barca'

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel, amethibitisha kuwa alimwondoa Marcos Alonso kwenye kikosi dhidi ya Everton Jumamosi kwa sababu anataka kujiunga na Barcelona.

90min ilifichua Ijumaa kwamba, Barca walikuwa na uhakika wa kumalizia dili la Alonso mwezi huu, na tuhuma kwamba mkataba ulikuwa karibu uliibuliwa wakati Alonso hakutajwa kwenye kikosi cha Chelsea kwa ajili ya mechi yao ya ufunguzi wa msimu Jumamosi.

Baada ya ushindi wa bao 1-0 pale kwenye dimba la Goodison Park, Tuchel alithibitisha kwamba, Alonso ameomba kuondoka na hivyo aliamua kuamuacha kuelekea mchezo huo.

Alipoulizwa iwapo Alonso aliomba kuondoka Stamford Bridge, Tuchel alisema: "Ndivyo ilivyo. Anajaribu kuondoka na tulikubaliana na matakwa haya. Ndiyo maana isingekuwa na maana kumweka uwanjani leo (juzi).

"Angekuwa uwanjani vinginevyo, lakini katika hali hii, lilikuwa jambo sahihi kufanya."

Wakati Alonso anataka kuondoka Chelsea na kwenda Barcelona, Cesar Azpilicueta amesitisha mipango yake ya kuhamia Camp Nou.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# OKWA: NAIJUA FALSAFA YA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI aliyesajiliwa na Klabu ya Simba msimu huu akitokea Rivers United ya kwao Nigeria, Nelson Okwa, amesema hatopata tabu kuingia kwenye mfumo wa uchezaji kwa sababu anaifahamu timu hiyo, aina ya uchezaji pamoja na wachezaji wao.

Akizungumza Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Okwa alisema amekuwa akiifuatilia Simba kabla ya kujiunga na anajua falsafa ya uchezaji wa timu hiyo, hivyo hatopata tabu yoyote ya kuingia kwenye mfumo, au kuzoeana na wenzake kwa sababu ameshajua jinsi gani ya kucheza akiwa ndani ya timu hiyo.

"Nina furaha kujiunga na Simba na nimefurahi kuwa hapa, nilikuwa nafuatilia mechi ya klabu hii kabla ya kuja. Ni timu kubwa, nilikuja hapa kucheza dhidi ya Yanga, nikaisikia klabu hii kwa ukaribu zaidi, lakini kabla ya hapo nilisikia walikuja nyumbani kucheza na Plateau, siku hiyo nilikuwa uwanjani kuwatazama, niliona kila kitu, niliona aina yake ya uchezaji, falsafa yao, ndiyo maana nilikubali kuja kucheza kwenye timu hiyo, kwa sababu najua mechi kuhusu wao," alisema mchezaji huyo.

**Simba ilicheza dhidi ya Plateau United Novemba 20, 2020 nchini Nigeria na kushinda bao 1-0 la Clatous Chama, na kwenye mechi ya marudiano Dar es Salaam, Desemba 5, zilitoka suluhu, Simba ikisonga mbele.**

Mchezaji huyo alikuja nchini kucheza dhidi ya Yanga Septemba 12, mwaka jana, wageni wakishinda bao 1-0 kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kabla ya timu yake kushinda tena nyumbani nchini Nigeria bao 1-0, Septemba 19, mwaka jana.

Taarifa kutoka ndani ya klabu ya Simba zinaeleza kuwa mchezaji huyo ndiye kwa kiasi kikubwa alishinikiza kutua kwenye timu hiyo, huku wakala wake akiwa anataka kumpeleka klabu zingine za nje ya nchi.

Okwa, mwenye uwezo wa kucheza nafasi ya winga na kiungo mshambuliaji, anatajwa kuwa ndiye anayekwenda kuziba nafasi ya Rally Bwalya ambaye ameondoka kwenda kujiunga na klabu ya Amazulu ya Afrika Kusini.




Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili (kulia), akimkabidhi zawadi ya kombe mshindi wa jumla wa mashindano ya Gofu ya Corporate Masters, Hussein Dewji, baada ya kuibuka mshindi wa fainali ya mashindano hayo yaliyofanyika Viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Benki ya CRDB ilikuwa miongoni mwa wadhamini wa mashindano hayo. Kushoto ni Meneja Mwandamizi Kitengo cha Wateja Maalum, Gibson Mlaseko. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Waziri Junior, Ame waibukia KMC*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imetangaza kuwasajili wachezaji 14 wapya wakiwamo nyota wa zamani wa Klabu za Simba na Yanga, Ibrahim Ame na Waziri Shentembo Junior.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imeeleza kuwa wachezaji hao wamesajiliwa kutokana na mapendekezo ya benchi la ufundi.

"Nilisema unapotaka kujenga timu ni lazima ufanye maamuzi magumu, tumeacha wachezaji wengi kwa sababu tulitaka kujenga timu imara, tumesajili haswa, tumesajili wenye ubora na hadhi ya kuichezea KMC, hatujasajili wachezaji changanyikeni, tumevunja mikataba kwenye klabu zao, hatujasajili wachezaji ambao wamemaliza mikataba na wapo huru, unazoa tu, hapana," alisema Ofisa Habari wa klabu hiyo, Christina Mwagala.

Wachezaji waliotangazwa ni Waziri Junior, straika aliyewahi kuichezea Yanga, msimu uliopita aliichezea Dodoma Jiji na Ibrahim Ame, beki wa zamani wa Simba, ambaye msimu uliomalizika alikuwa akikipiga dhidi ya Mtibwa Sugar.

Wengine ni Baraka Majogolo kutoka Mtibwa Sugar, Isack Kachwele, Mrundi, Blaise Bigirimana wa Namungo, Styve Nzigamasabo kutoka Mtibwa Sugar, Boniphace Maganga kutoka Biashara United, Daruweshi Saliboko aliyesajiliwa kutoka Polisi Tanzania, David Kissu aliyekuwa akiidakia Azam FC, Nourdine Ballora kipa raia wa Burkina Faso aliyezichezea klabu ya Namungo na Biashara United, Erick Costantine, Farshad Mogella na Balisi Maliki.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 08/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3273 | Gyeongnam vs Anyang | 2.29 | 3.40 | 2.71 |
| 13:00 | 4908 | Jeonnam Dragons vs Bucheon | 2.26 | 3.14 | 2.95 |
| 16:30 | 2635 | Shirak Gyumri vs Urartu | 3.14 | 3.24 | 2.11 |
| 18:00 | 1215 | Neftekhimik vs Rubin Kazan | 3.34 | 3.44 | 1.96 |
| 18:00 | 1815 | Spartaks Jurmala vs BFC Daugavpils | 2.16 | 3.50 | 2.86 |
| 18:00 | 3542 | Hermanstadt vs Voluntari | 2.31 | 3.04 | 3.14 |
| 18:00 | 5845 | Lahti vs Hifk | 1.83 | 3.54 | 3.69 |
| 18:30 | 3615 | Klubi 04 vs Tampere United | 1.41 | 4.93 | 5.32 |
| 18:45 | 1692 | Genoa vs Benevento | 1.99 | 3.47 | 3.52 |
| 19:00 | 1626 | Aasane Fotball vs Fredrikstad | 2.60 | 3.34 | 2.40 |
| 19:00 | 2068 | Ranheim vs Mjondalen | 1.79 | 3.59 | 3.79 |
| 19:00 | 2513 | IK Start vs Bryne | 1.49 | 4.33 | 5.11 |
| 19:00 | 2839 | Grorud IL vs Kongsvinger IL | 2.75 | 3.59 | 2.18 |
| 19:00 | 3244 | ZKS Stal Rzeszow vs Ruch Chorzow | 2.16 | 3.14 | 3.14 |
| 19:00 | 3292 | Sandnes Ulf vs Skeid Fotball | 1.60 | 3.88 | 4.61 |
| 19:00 | 4063 | Strindheim IL vs Rosenborg BK 2 | 2.00 | 4.33 | 2.71 |
| 19:00 | 5389 | Modena vs Sassuolo | 3.27 | 3.37 | 2.11 |
| 19:15 | 3217 | Basaksehir vs Kasimpasa | 1.81 | 3.57 | 4.12 |
| 19:30 | 1199 | Ceramica Cleopatra vs Enppi Club | 2.34 | 2.86 | 3.36 |
| 19:30 | 1862 | Talaea El Gaish vs Eastern Company SC | 1.87 | 3.22 | 4.33 |
| 20:00 | 1727 | Baltika Kaliningrad vs Arsenal Tula | 2.80 | 3.34 | 2.26 |
| 20:00 | 1771 | Asker vs Valerenga IF 2 | 1.60 | 4.42 | 4.02 |
| 20:00 | 2490 | AFC Eskilstuna vs Jonkopings Sodra | 1.96 | 3.72 | 3.57 |
| 20:00 | 2609 | Vasteras SK vs Brommapojkarna | 2.95 | 3.56 | 2.27 |
| 20:00 | 2647 | Orebro SK vs Orgryte IS | 2.01 | 3.61 | 3.51 |
| 20:00 | 3117 | Silkeborg vs Aalborg | 1.74 | 3.87 | 4.13 |
| 20:00 | 3404 | BK Hacken vs Helsingborg | 1.33 | 4.93 | 6.90 |
| 20:00 | 3847 | Penafiel vs Leixoes | 2.20 | 3.15 | 3.20 |
| 20:00 | 5037 | Javor Ivanjica vs FK Mladost Gat Novi Sad | 2.13 | 3.10 | 3.24 |
| 20:00 | 5168 | Wisla Plock vs Miedz Legnica | 1.70 | 3.53 | 4.41 |
| 20:00 | 5327 | Varbergs Bois vs IFK Goteborg | 2.80 | 3.30 | 2.27 |
| 20:30 | 3871 | Dudelange vs Jeunesse Esch | 1.53 | 4.23 | 4.72 |
| 21:00 | 2196 | Botosani vs Farul Constanta | 2.55 | 3.10 | 2.75 |
| 21:00 | 3550 | Albion FC vs Liverpool (URU) | 3.87 | 3.48 | 1.80 |
| 21:00 | 4409 | Gimnasia Jujuy vs Quilmes | 2.21 | 3.04 | 3.13 |
| 21:00 | 4874 | Jong AZ Alkmaar vs Maastricht | 1.84 | 3.77 | 3.63 |
| 21:00 | 5636 | Jong Ajax vs Telstar | 1.60 | 4.20 | 4.50 |
| 21:10 | 3491 | Racing Club vs CA Huracan | 1.29 | 5.32 | 7.29 |
| 21:15 | 5491 | Diosgyori Vtk vs Soroksar | 1.62 | 3.79 | 4.53 |
| 21:15 | 5629 | ND Gorica vs Luka Koper | 3.58 | 3.29 | 1.93 |
| 21:45 | 3082 | Fenerbahce vs Umraniyespor | 1.28 | 5.43 | 9.25 |
| 21:45 | 3928 | Ankaragucu vs Konyaspor | 3.12 | 3.42 | 2.16 |
| 21:45 | 4968 | Caen vs Metz | 2.51 | 3.01 | 2.86 |
| 22:00 | 3955 | Cremonese vs Ternana | 1.75 | 3.66 | 4.31 |
| 22:00 | 5681 | West Bromwich vs Watford | 2.35 | 3.10 | 3.00 |
| 22:15 | 2326 | IA Akranes vs Valur | 4.24 | 3.84 | 1.66 |
| 22:15 | 2544 | Gil Vicente vs Pacos Ferreira | 1.75 | 3.47 | 4.63 |
| 22:15 | 3356 | Bologna vs Cosenza | 1.50 | 4.11 | 6.01 |
| 22:15 | 5858 | Leiknir vs Keflavik IF | 2.65 | 3.59 | 2.25 |
| 23:00 | 5485 | Real Santander vs Bogota FC | 1.58 | 3.76 | 4.95 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Agosti 8, 2022

Nipashe




Klopp alia Liver kuanza vibaya UKURASA 21

UZI MPYA...



Pape Sakho Shomari Kapombe Jonas Mkude

## Nabi akiri Yanga bado

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema anahitaji muda zaidi wa kutengeneza timu yake kwa kujenga muunganiko mzuri kati ya wachezaji wapya na wale waliobakia wa msimu uliopita baada ya kuona udhaifu wao kupitia mechi ya kirafiki dhidi ya Vipers ya Uganda.

Hayo aliyazungumza juzi baada ya mchezo wa Yanga wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Vipers iliyoshinda mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema mechi hiyo imekuwa kipimo kizuri kwa timu yake na amepata mwanga wa kuona baadhi ya vitu ambavyo anaenda kuvifanyia kazi.

Alisema ameona mapungufu ya kikosi chake, hivyo anahitaji kupata muda wa kutosha wa kutengeneza timu kwa wachezaji wapya na wazamani kupata nafasi ya kutengeneza muunganiko mzuri.

"Matokeo ya mechi yetu si mazuri, lakini kwangu nafurahi kuona nimepata kipimo tosha na vitu ambavyo natakiwa kufanyia kazi, wachezaji wapya na waliokuwapo msimu uliopita hawajapata muda wa kutosha wa kutengeneza muunganiko mzuri," alisema Nabi.

# Simba haijawahi kutokea

**Na Saada Akida**

## Mabomu yarindima wakigombania kununua jezi, straika Dejan asaini rasmi, Manzoki asema narudi...

JEZI za msimu mpya za Klabu ya Simba zimeweka rekodi kwa mashabiki wa soka kugombea kununua hadi Jeshi la Polisi kulazimika kutumia mabomu ya machozi kuwatawanya katika duka la mdhamini wa jezi hizo, Fred Vunjabei lililoko Sinza Madukani, Dar es Salaam.

**Mashabiki wa Simba jana walitia fora baada ya kumiminika kwa wingi katika duka la Vunjabei wakitaka kununua jezi mpya kwa ajili ya Tamasha lao la Simba Day leo.**

Mzigo huo ulianza kuuzwa rasmi jana baada ya kuchelewa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kubadili mdhamini kutoka SportPesa na kuingia mwingine ambaye ni M-BET zoezi ambalo lilifanya kuchelewa kuwasili.

Kutokana na umati huo na kila mmoja kuhitaji kuingia ndani kupata nafasi ya kununua jezi hizo mpya, ilisababisha tafrani na vurugu kwa mashabiki hao, hivyo kusababisha watu wa usalama kupiga bomu la machozi ili kuleta utulivu.

Pamoja na jezi hizo kuchelewa kuingia sokoni, lakini mashabiki wa timu hiyo walionekana kuvutiwa zaidi kila mmoja akitamani kubeba aina zote tatu licha ya kutakiwakununua moja moja ili kila mmoja aweze kupata.

Mmoja wa mashabiki waliojitokeza dukani hapo, Rashid Mtambo, alisema misimu yote Simba wanakuwa na jezi kali ila ya msimu huu ni balaa zaidi.

"Simba huwa hatuna jambo dogo, miaka yote tumekuwa na jezi kali ila ya msimu huu ni zaidi ya balaa na unaweza kutinga na kwenda nayo kwa wakwe zako," alisema Rashid.

Katika hatua nyingine Simba imemtambulisha mshambuliaji mpya raia wa Serbia, Dejan Georgijevićaliyekuwa akichezea NK Domžale ya Slovenia.

Dejan mwenye umri wa miaka 28, ambaye amefunga mabao manne katika mechi 17 za msimu uliopita, amesaini mkataba wa miaka miwili kuichezea Simba na atakuwa miongoni mwa wachezaji watakaotambulishwa leo katika Tamasha la Simba Day kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwingineko mshambuliaji wa Vipers ya Uganda, Cesar Manzoki, ambaye alitarajiwa kutua Simba, aweka wazi kuwa amebakiza mkataba wa miezi miwili unaofikia tamati Oktoba mwaka huu na sio 2025 kama waajiri wake hao wanavyodai.

Manzoki anatajwa kumalizana na klabu ya Simba huku uongozi wa Vipers kupitia Ofisa Habari wao, Wasike Abdu, akidai kwamba nyota huyo bado ni mchezaji wao halali kwa kuwa wana mkataba naye hadi 2025.

Akizungumza na gazeti hili jana Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, kabla ya timu ya Vipers kuelekea nchini kwao Uganda, Monzoki, alisema hakuna ukweli juu ya mkataba wake na kwamba ulikuwa wa miaka miwili ndani ya klabu yake ya sasa ambao unamalizika Oktoba.

Alisema Meneja wake na viongozi wa Simba wako mezani wanazungumza kwa ajili ya kusaini mkataba kuitumikia klabu hiyo na tayari wamepeleka barua Vipers kwa ajili ya kununua mkataba wake kwa muda uliobakia.

"Huo sio ukweli kwamba mkataba wangu ni miaka miwili ndani ya Vipers, nimebakiza miezi miwili na Oktoba namaliza na klabu yangu, lakini kuhusu Simba, meneja wangu na Simba wako katika mazungumzo mazuri.

"Malengo yangu ni kucheza Simba, kama mambo yakienda vizuri basi nitakuwa sehemu ya kikosi cha timu hiyo, kuhusu kutocheza mechi dhidi ya Yanga ni kwa sababu ya kutojisikia vizuri," alisema Manzoki ambaye alikuwa hapa nchi na timu yake ya Vipers kwa mchezo wa kirafiki dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na wageni hao kushinda mabao 2-0.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >